

**MWINYI:** Hapa ndipo jina Mzee Rukhsa lilipoanzia

UKURASA 4

**KILIMO** yatoa vipaumbele saba kuleta mapinduzi

UKURASA 3


Nipashe TESA
Jumanne Mei 25, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Ukurasa 14
Ukurasa 12
Wanaowahudumia wenye ulemavu wanasema haya...
Taasisi yataja ulipo uwezeshaji endelevu kwa kaya maskini
ELIMU
NA NIMI MWETA
HELSB NI MZIGO
Vinahitajika vyanzo, vigezo ushahidi mujarabu kuifuta
Shughuli za mahafali katika moja ya vyuo vya elimu ya juu. PICHA: MTANDAO.

SHUGHULI za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) hazina ufanisi kwani gharama za uendeshaji wake na mapungufu yanayoambatana nayo yanazidi faida za uwepo wa chombo hicho na anadhani njia pekee ni kuifuta.'

Ni maoni ya aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ludovick Utouh.

Anayaeleza hayo kwenye jukwaa moja lililokuwa linajadili ripoti ya mwaka 2020 ya CAG iliyotolewa kuelekea mwisho wa mwezi Machi mwaka huu na kuzua mijadala maridhawa hasa bungeni. Lakini katika mahojiano na gazeti hili.

Katika kuitafakari kauli ya Utouh pengine maswali kadhaa yanaibuka mfano, elimu ya vyuo vikuu bila mikopo inawezekana au ni lazima lea na masomo ya elimu ya juu? Ni jambo gani linaweza kufanyika ili kuwepo na taasisi ya kusimamia mikopo hiyo?

Pengine, siyo rahisi kusema kuwa hisia hiyo ya CAG ni rahisi kukubaliwa kila mahali au miongoni mwa wataalamu kwa jumla, kwani mambo yanabadilika kulingana na wakati uliopo. Anachosema Utouh kilikuwa 'kweli' zaidi katika kipindi alichokuwa akiondoka madarakani au kuelekea mwisho wa awamu ya nne, na miaka michache iliyofuata. Hii ndiyo picha inayojitokeza katika kuangalia baadhi ya taarifa pembuzi za wakati huo, kwa mfano mojawapo ilichapishwa Septemba 4, 2016, ikisema kuwa vyuo vikuu vya Tanzania vina tatizo kubwa la mikopo kwa wanafunzi hewa, ililivalia njuga na kuelekea kulimaliza.

Wakati huo, serikali ilisimamisha mikopo ya wanafunzi takribani 2,000 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.2 baada ya zoezi la kuyakinisha utolewaji wa mikopo kubaini kuwa baadhii ya wanafunzi waliopewa fedha hizo walikuwa hewa. Kwa vile idadi ya wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu inazidi 100,000 uwepo wa mikopo 2,000 yenye hitilafu inaweza kuonekana ni jambo dogo, lakini fedha za mikopo zinafujwa, kwa kudhamiria au kutokana na uongozi hafifu, hivyo kuathiri mfumo mzima wa elimu ya juu na mwishowe, taifa linalotoa fedha hizo. Kimsingi ndicho alichoainisha CAG katika mada yake.

Ila kwa nyakati tofauti ... uhai na ufanisi wa mpango wa mikopo ya elimu ya juu na urudishwaji wake, ukiangalia taarifa iliyochapishwa Machi 21, 2019 mitandaoni na mashirika ya habari ya kimataifa, yakinukuu habari za hapa nchini. Taarifa hiyo iligusia kuongezeka kwa haraka kwa ufanisi katika miezi kadhaa iliyotangulia kwa suala la ukusanyaji malipo kwa wafaidika wa mikopo ya elimu ya juu, ambako kiasi cha wanafunzi 5,000 wapya wangepata mikopo katika mwaka huo wa fedha kutokana na kasi ya urudishaji. Moja ya sababu ni makato zaidi katika mishahara ya wafaidika.

Ukisikiliza alichosema Utouh na kilichojiri hivi karibuni wakati Rais Samia Suluhu Hassan, anachukua uongozi wa taifa kwa ...

Mosi, kinachoonekana ni kuwapo mgongano wa hisia na mapendekezo nini kifanyike katika eneo hilo. Utouh anaonekana kukata tamaa kuhusu kuleta ufanisi katika eneo hilo, kwa msingi ule ule alioeleza kuhusu maeneo mengine ambako bodi hazifanyi kazi. Itakumbukwa kuwa Rais Samia aliagiza bodi za wafanyakazi ambazo pia zinahusika kuangalia maslahi ziundwe katika sekta tofauti au zianze kufanya kazi, ila kwa vile mishahara haipandi zilikuwa zimeichoka.

Hata hivyo Rais Samia hakukubali pendekezo la kupunguzwa kwa kiwango kinachokatwa katika mshahara wa mfaidika ili kulipia mkopo wa elimu ya juu, lakini akafuta riba ya asilimia sita iliyokuwa ikiongezwa kuendana na urudishwaji wa mikopo kwa kuchelewa. Ukiongeza kasi ya kurudisha ambayo tayari ilishaonekana, inaelekea kuwa hapo kuna suala la usimamizi, hivyo mwelekeo wa fikra ya CAG mstaafu kuwa mfumo wa mikopo ufumuliwe bado haikidhi mahitaji. Kwa nchi kama Tanzania ambako elimu ya juu ni gharama kubwa, si wazo baya kuhitaji waliofaidika kulipa zaidi kuwezesha elimu ya juu kwa wengine kwa njia ya mikopo, kwa msingi kuwa gharama za usimamizi wa suala hilo ziwe endelevu.

Endapo usimamizi na uongozi wa mikopo ni mbovu, wakuu wa vyuo au maofisa wa bodi wanafuja fedha za mikopo hewa, halafu bodi imejaa ajira zisizoeleweka, kama Utoah unaweza kusema kuwa mpangilio huo umeshindwa.

Suala hapa ni kuwa Utoah ana haki ya maoni yake lakini hakuna vyanzo vya kutosha kuyakinisha hoja kuwa ni kweli ufanisi wa mfumo wa bodi ya mikopo ni mdogo mno na hakuna haja ya kuendelea nao.

Ni wazi kuwa hisia hiyo bado ni changu ni ya wasomi zaidi na hasa wale wenye uwezo wa kupitia kwa kina nyaraka husika ikiwamo ripoti ya ukaguzi wa hesabu za serikali. Waliobaki ambao ni Watanzania ...

UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Mei 25, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580591

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710


# MATUMAINI MAPYA

## RAIS Samia aagiza kiwanda cha Dangote kazi iendelee, mwenyewe ahaidi makubwa...*Endelea Ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 4**


### WAZIRI MKUU ASISITIZA UTAFITI, UBUNIFU

SERIKALI imesisitiza masuala ya utafiti na ubunifu kutiliwa mkazo na kuwekewa utaratibu maalumu...

**UKURASA WA 5**

### WFP YAIPATIA TASAF BIL. 1.6/-

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wamesaini mkataba...

Rais Samia Suluhu Hassan akiwa katika mazungumzo na mmiliki wa Kiwanda cha Saruji cha Dangote, Alhaji Aliko Dangote, baada ya kuwasili Ikulu jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: IKULU**

## TEMBO 200 WAINGIA MTAANI

UKURASA 2

# RC asimulia Rais Samia alivyomkosesha usingizi

UKURASA 5


**MICHEZO** **SIMBA YAPANIA KUISHUSHIA HASIRA DODOMA JIJI FA CUP** UK. 23

**MAONI, KATUNI UK. 6**



Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroth Gwajima, akiangalia mfumo wa kuwahudumia wagonjwa uliopo Hospitali ya Rufani Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# MATUMAINI MAPYA DANGOTE

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ameziagiza Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Fedha na Mipango, kufanyia kazi changamoto zote zinazokikabili kiwanda cha kuzalisha saruji cha Dangote, ili kiendelee na uzalishaji na kuleta manufaa yaliyokusudiwa.

Rais Samia alitoa agizo hilo jana, alipokutana na kufanya mazungumzo na mfanyabiashara Alhaji Aliko Dangote, ambaye amewekeza katika kiwanda kikubwa cha uzalishaji wa saruji mkoani Mtwara.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Gerson Msigwa, kwa vyombo vya habari, ilisema kuwa, Rais Samia alimtaka Waziri wa Viwanda na Biashara, Kitila Mkumbo na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Masauni, waliohudhuria mazungumzo hayo, kuzifanyia kazi changamoto zote zinazokikabili kiwanda hicho ili kiendelee kufanyakazi kinavyotakiwa.

Katika maongezi hayo Alhaji Dangote, amempongeza Rais Samia kwa kuchukua hatua mbalimbali za kuboresha mazingira ya biashara nchini Tanzania na amemwahidi kuwa kampuni yake ambayo imewekeza nchini kiasi cha Dola za Marekani milioni 770 (Sh. trilioni 1.761), itaendelea kuwekeza katika maeneo mengine ikiwamo mpango wake wa kujenga kiwanda cha kuzalisha mbolea.

"Tutaendelea kuwekeza Tanzania ili kuzalisha ajira, mapato ya nchi na kuinua ustawi wa wananchi wa Tanzania, nadhani anahitaji kuungwa mkono katika hili na tumemwahidi kuwa tutaendelea kuwekeza kwa kiasi kikubwa hapa Tanzania ili kuunga mkono anachokifanya, sisi tutazalisha ajira," alisema Alhaji Dangote.

**Tutaendelea kuwekeza Tanzania ili kuzalisha ajira, mapato ya nchi na kuinua ustawi wa wananchi wa Tanzania, nadhani anahitaji kuungwa mkono katika hili na tumemwahidi kuwa tutaendelea kuwekeza kwa kiasi kikubwa hapa Tanzania ili kuunga mkono anachokifanya, sisi tutazalisha ajira," alisema Alhaji Dangote.**



Alisema kutokana na kubadilika na kuimarika kwa mazingira ya biashara nchini Tanzania, atawahimiza wafanyabiashara na wawekezaji wenzake kuwekeza Tanzania kwa kuwa serikali ipo tayari kushirikiana nao.

Kwa upande wake, Rais Samia alimpongeza Alhaji Dangote kwa uwekezaji alioufanya hapa nchini na amemhakikishia kuwa serikali itahakikisha uwekezaji wake na wawekezaji wengine unalindwa kwa manufaa ya pande zote mbili.

**KIWANDA CHA DANGOTE**

Kiwanda cha Dangote kilizinduliwa nchini mwaka 2015 na kufanya uwekezaji mkubwa katika saruji kuliko viwanda vyote Afrika Mashariki.

Kiwannda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani milioni tatu kwa mwaka na kutoa ajira ya moja kwa moja kwa zaidi ya watu 1,000 wa Mtwara.

Dangote ni tajiri namba moja Afrika ambaye hadi Juni mwaka 2016, alikuwa akikadiriwa kuwa na utajiri wa Dola za Marekani 14.9 bilioni sawa na Sh. trilioni 32.33.

Mfanyabiashara huyo alianzisha kampuni ya Dangote mwaka 1981 ikiwa na makao yake makuu nchini Nigeria ikijihusisha na biashara tofauti na kuzalisha saruji.

Kampuni hiyo inafanya biashara katika nchi 16 Afrika ambazo ni Tanzania, Zimbabwe, Kenya, Nigeria, Niger, Senegal, Afrika Kusini, Sierra Leone, Mali, Liberia, Ghana, Ethiopia, Cameroon, Congo na Ivory Coast na Nepal.

# Tembo 200 waingia mtaani

**Na Zainab Omary, UDOM**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amewatahadharisha wakazi wa Mkoa wa Ruvuma baada ya picha ya satelite kuonyesha tembo zaidi ya 200 wapo nje ya hifadhi.

Aliwataka wananchi wasishangae kuyaona makundi ya tembo hayo karibu na makazi yao.

Dk. Ndumbaro aliyasema hayo baada ya kuwatembelea wakazi wa Wilaya ya Tunduru na Namtumbo, mkoani Ruvuma na kuzungumza na wakazi wa vijiji sita vilivyoathiriwa zaidi na tembo hao.

Kadhalika, Waziri Ndumbaro alisema ametembelea eneo hilo, ili kujibu kero mbalimbali zinazotokana na uvamizi wa wanyama hao katika maeneo yao wakitokea Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere.

"Tembo zaidi ya 200 wapo nje ya Hifadhi Taifa ya Mwalimu Nyerere kutokana na wafugaji kuingiza makundi ya n'gombe ndani ya hifadhi hiyo.

"Wenyeviti wa vijiji wamekuwa wakiwakaribisha wafugaji kutoka katika mikoa mbalimbali kuhamia katika maeneo ya vijiji, kisha kuingiza mifugo hiyo ndani ya hifadhi kwa ajili ya kupata malisho," alisema Dk. Ndumbaro.

Alisema utafiti uliofanywa kwa njia ya satelite hivi karibuni ulionyesha tembo hao wapo nje ya hifadhi na kuwataka wananchi wachukue tahadhari pamoja na kutoa taarifa wanapoona makundi ya wanyama hayo yakiwa karibu na makazi.

Pia alisema ng'ombe kuingia ndani ya hifadhi husababisha, tembo kutoka nje ya hifadhi, kutokana na kutopenda kuchanganyana na mifugo au watu.

"Tembo hawapendi kuchangamana na ng'ombe kutokana na harufu ya dawa wanayotumia kuoshewa katika majosho."

Aliagiza wafugaji walioingiza ng'ombe ndani ya hifadhi hiyo walipe faini, wataifishwe na wasipouzika wapatiwe Jeshi la Magereza kwa ajili ya kitoweo kwa wafungwa.

Aidha, Waziri Ndumbaro alitaja sababu nyingine iliyochangia tembo kutoka nje ya hifadhi ni tabia ya baadhi ya wananchi kulima kwenye kingo za hifadhi hali inayowavutia kutoka nje kwa ajili ya kula mazao.

"Idadi ya mashamba pamoja na wananchi kujeruhiwa inazidi kuongezeka siku hadi siku, si kwa sababu idadi ya tembo imeongezeka, bali ni kutokana na idadi ya watu kuongezeka na kulazimika kufanya shughuli ndani ya hifadhi," alisema Dk. Ndumbaro.

Kadhalika, aliwaonya wananchi kuacha kulima katika hifadhi za wanyamapori, huku Mbunge wa jimbo hilo, Vita Kawawa, akiomba kwa waziri wananchi wa Namtumbo waliathiriwa na tembo wanaovamia makazi na mashamba yao, wizara iwalipe kifuta machozi.

Mbunge wa Tunduru Kaskazini, Hassan Kungu, alimwomba Waziri Ndumbaro kuongeza fedha za vifuta machozi, kwa sababu fedha wanayolipwa wananchi hailingani na thamani ya mashamba yaliyoharibiwa na tembo.

HABARI KITAIFA

# ACT-Wazalendo yatoa mapendekezo kwa Samia

**Na Enock Charles**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetoa mapendekeo manne kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kikitaka kufanyiwa maboresho, mojawapo ni kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi ambayo itakuwa na watumishi wasiokuwa makada wa chama cha siasa.

Kimesema tume ya sasa ina watumishi ambao ni makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), hivyo kutokuwa huru.

Mapendekezo hayo yametolewa jana na Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe na kuwekwa kwenye akaunti za mitandao ya kijamii za chama hicho.

Sehemu ya taarifa hiyo ilieleza kuwa: "Tunapendekeza kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) iwe na watumishi wake wanaowajibika kwa tume, tena wasiwe ni makada wa chama kimoja cha siasa."

Chama hicho pia kimependekeza kupitiwa upya kwa Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuleta uhuru kwa vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, ambayo wamedai kuzuiwa kuifanya na sababu ikiwa ni sheria hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa: "Rais Samia Suluhu Hassan aanzishe mchakato shirikishi wa kupitia upya Sheria ya Vyama vya Siasa ili kuondoa vifungu vyote vinavyojinaisha siasa na kubana uhuru wa vyama vya siasa kutekeleza majukumu yake.

"Tunaomba vyama vya siasa virejeshewe haki yake ya kisheria ya kufanya mikutano yake bila bugudha."

Kadhalika kimependekeza kupitia taasisi zinazomilikiwa na vyama vya siasa kama vile Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), Rais Samia aanzishe majadiliano miongoni mwa vyama ili kujenga kuaminiana na kutatua migogoro kwa njia ya amani pale inapotokea.

Chama hicho kimependekeza kuwapo unasihi wa vyombo vya ulinzi na usalama kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia sheria na kulingana na viapo vyake, kutojiingiza katika itikadi za kisiasa.

Chama hicho pamoja na vyama vingine vya upinzani ikiwamo Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Chama cha NCCR-Mageuzi na Chama cha Wananchi CUF kwa muda mrefu vimekuwa vikidai kuwapo kwa tume huru ya uchaguzi.

Katika uchaguzi mdogo wa marudio wa hivi karibuni katika majimbo ya Muhambwe na Buhigwe mkoani Kigoma, CHADEMA ilisusia uchaguzi huo ikitaka kufanyike marekebisho kwenye tume ya uchaguzi.



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi (kulia), akimkabidhi vitabu vya ofisi Mkuu wa Mkoa wa Iringa mpya, Queen Sendiga, wakati wa makabidhiano ya ofisi mjini Iringa jana. Hapi amehamishiwa Mkoa wa Tabora. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Vipaumbele 7 mapinduzi kilimo nchini

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo imeweka vipaumbele saba kwa ajili ya kuongeza tija katika uzalishaji, kikubwa kikiwa ni cha kimkakati ya mkazo katika utafiti utakaozingatia ugunduzi wa aina za mbegu bora na mbinu bora za kilimo.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, aliyesema hayo jana wakati akiwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2021/22.

Alisema kipaumbele cha kwanza ni kufanya utafiti wa mbegu bora zenye tija kubwa kwa mfano utafiti unaonyesha kuwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imefanikiwa kugundua aina za mbegu za muhogo zinazozalisha wastani wa tani 22-50 kwa hekta ikilinganishwa na wastani wa tani nane kwa hekta zinazozalishwa sasa na wakulima wengi.

Alisema kwa upande wa pamba, tija ya sasa ni kilo 250-300 kwa ekari ikilinganishwa na uwezo wa kufikia wastani wa kilo 1,000-2,000 kwa ekari na kwamba wataongeza bajeti ya TARI kutoka Sh. bilioni 7.35 mwaka 2020/2021 hadi Sh. bilioni 11.63 mwaka 2021/2022.

Alisema pia wataimarisha upatikanaji wa fedha za maendeleo ya utafiti wa kilimo kwa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Utafiti kwa mujibu wa sheria.

Kipaumbele cha pili, ni kuongeza uzalishaji wa mbegu bora kutokana na nchi kutojitosheleza kwa mahitaji ya mbegu na kulazimika kuagiza kutoka nje ya nchi, na Wizara itaendeleza mashamba 13 ya mbegu ya ASA kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji kwa kutumia fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji.

Kipaumbele cha tatu ni kuimarisha huduma za ugani kwa kuwa hadi sasa maofisa ugani wanaotoa huduma za ugani nchini katika ngazi ya kata na vijiji ni 6,704, ambayo ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji ya 20,538.

Aidha, alisema wizara itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha huduma za ugani kwa kutumia mbinu zilizoonyesha mafanikio katika kuongeza tija.

Cha nne, ni kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na kuondokana na kilimo cha kutegemea mvua ambazo hazitabiriki.

Kipaumbele cha tano, ni kuimarisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo na changamoto iliyopo ni uzalishaji mdogo usiokidhi mahitaji ya soko na kuwapo kwa uzalishaji mkubwa ikilinganishwa na upatikanaji wa masoko.

Alisema serikali itaimarisha utekelezaji wa kilimo cha mkataba katika mazao ya shayiri, ngano, alizeti, zabibu, maharage ya soya na mazao mengine kwa kutoa mwongozo wa mikataba baina ya wakulima na wenye viwanda vya kusindika mazao.

Pia kilimo cha ubia wa kibiashara baina ya wafanyabiashara wa mazao hapa nchini na nchi za nje zenye fursa kubwa ya masoko ikiwamo Sudani Kusini, DRC, Saudi Arabia, Falme za Kiarabu, Msumbiji, Kenya, Vietnam na China.

Cha sita, ni kuimarisha kilimo unga kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya milipuko na vihamavyo kama vile nzige, kwelea kwelea na viwavijeshi vamizi, ambao wamesababishwa na mabadiliko ya tabianchi kiasi cha kuwa na ongezeko la visumbufu vigeni vinavyoathiri uzalishaji wa mazao na kusababisha upotevu wa mazao hadi asilimia mia moja endapo havitadhibitiwa kikamilifu na kwa wakati.

Kipaumbele cha saba ni kuimarisha mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya shughuli za kilimo na kwamba kikwazo kikubwa ni riba kubwa zinazotozwa, masharti ya kupata mikopo kutoka taasisi za fedha.

"Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa ni asilimia 30 tu ya wakulima wanaofikiwa na huduma za mikopo. Ni asilimia kati ya saba na tisa ya mikopo iliyotolewa na benki ya biashara katika kipindi cha miaka mitano iliyopita imeelekezwa kwenye sekta ya kilimo," alisema.

Waziri Mkenda alisema mwaka 2021/2022, wizara itafanya tathmini ya mifumo ya upatikanaji wa mitaji kwa wakulima wadogo na wawekezaji wengine kwenye sekta ya kilimo ili kuibua vizuizi na kuvitafutia majawabu kwa ajili ya kuimarisha ugharamiaji wa mazao katika mnyororo wa thamani.


NMB Karibu yako

**MABORESHO YA MAWASILIANO NA TAARIFA ZA KIBENKI KWA WANAHISA WA BENKI YA NMB KWA AJILI YA MALIPO YA GAWIO**

Benki ya NMB Plc inaendelea na juhudi za kuhakikisha wanahisa wetu wanaridhika na huduma zetu na malipo ya gawio kwa wakati. Gawio hulipwa kupitia akaunti za benki za wanahisa. Tunaomba wanahisa wote wa NMB waboreshe taarifa za mawasiliano yao na taarifa za kibenki kwa ajili ya akaunti zao husika watakazotumia kupokea gawio.

Hii ni kwa wanahisa pekee wa NMB;

i. Ambao hawajawahi kupata gawio lolote tangu waliponunua hisa
ii. Ambao waliobadilisha akaunti zao za kupokelea gawio na hawajaiarifu benki (Ikiwa ni pamoja na wanahisa wapya).
iii. Ambao wamebadilisha anwani zao za mawasiliano (namba za simu au anuani ya makazi)
iv. Ambao akaunti zao zimelala (Dormant) au kufungwa

Tafadhali tembelea tawi la NMB lililo karibu nawe na ujaze kwa usahihi fomu ya gawio la mwanahisa, na kisha uiwasilishe pamoja na kitambulisho na cheti cha hisa kwa dawati la huduma kwa wateja au tuma kama barua au barua pepe katika anuani zifuatazo hapo chini:

NMB Plc – Makao Makuu | Ohio/Ali Hassan Mwinyi
Ghorofa ya nne - Idara ya Fedha na Taarifa
S.L.P 9213, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 222 322 000 | Nukushi: +255 222 112 148

**Kwa maelezo Zaidi, tafadhali wasiliana nasi kupitia:**
Barua Pepe: Dividend_Unit@nmbbank.co.tz Au wasiliana moja kwa moja na:

- Njabha Njabha - Simu namba 0222 322 356
- Lucky Kyando - Simu namba 0222 322 421
- Robert Mwita - Simu namba 0222 322 376

www.nmbbank.co.tz

## Mwinyi: Hapa ndipo jina 'Mzee Rukhsa' lilipoanzia

**Na Christina Mwakangale**

RAIS mstaafu wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, anasimulia jinsi ambavyo hatasahau nchi ilivyopitia kwenye uhaba wa chakula na mafuta kwa wakati mmoja muda mfupi baada ya kuingia madarakani.

Katika simulizi ya kitabu chake cha 'Mzee Rukhsa, Safari ya Maisha Yangu', Mzee Mwinyi anaitafsiri kuwa ni aina ya mtikisiko wa nchi ilioupata ambao historia ya aina hiyo haijawahi kushuhudiwa tangu nchi ipate uhuru, mwaka 1961.

Anasema mwanzoni mwa miaka hiyo, uchumi wa Tanzania haukuwa mzuri, ndipo ilipoamua kuruhusu wafanyabiashara kununua na kuuza bidhaa kwa wananchi na ndio chanzo cha yeye kuanza kuitwa 'Mzee wa Rukhsa'.

"Mwaka 1983 upungufu wa chakula hasa mijini ulifikia hali mbaya kiasi ambacho chama (CCM), kililazimika kuweka utaratibu wa mfumo wa kugawa chakula kidogo kilichokuwapo," anasema Mzee Mwinyi.

Anasema kutokana na hali hiyo, mkoani Dar es Salaam makatibu tarafa wa chama, walipewa jukumu na Shirika la Taifa la Ugawaji kugawa chakula kwa wenye maduka ambao walikuwa na orodha ya wananchi.

Mwinyi anasema kila mkuu wa kaya alipewa kadi ya mgawo (resheni), ikionyesha anachostahili kupata na kila mtu alipangiwa nusu kilo ya nafaka, kwa siku.

"Mwanzoni utaratibu huu ulipunguza usumbufu...baada ya muda ikabainika hali haikuwa nzuri kiasi hicho, walianza kujitokeza wadanganyifu upande wa wenye maduka na wakati mwingine viongozi wa chama," anasimulia Mzee Mwinyi kwenye kitabu hicho.

Tatizo lilijitokeza kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio rasmi ambao walifanya ulanguzi wa bidhaa, kwa kununua vitu na kwenda kuviuza maeneo yaliyo na uhaba.

Anasema kampeni ilianzishwa kubaini waliokuwa na chakula kingi na kutiwa mbaroni kwa kosa la ulanguzi na kwamba aliwahi kubainika mtu mmoja aliyekutwa na gunia la mahindi lenye ujazo wa kilo 100.

"Ni wazi kuwa bei kubwa ya mazao ni kichocheo muhimu kwa mkulima kuongeza juhudi na uzalishaji. Lakini sisi katikati ya uhaba mkubwa wa chakula, tukapiga marufuku wakulima kuuza kwa bei juu, wengine wakaamua kulima kidogo tu kujitosheleza na familia zao," anasema Mwinyi.

"Wakati wa miaka ya 1980, wachumi mbalimbali wakiwamo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), wakaanza kuishauri serikali kuwa iondoe udhibiti wa bei ya mazao ya chakula, waweke vivutio vya wananchi kuzalisha." Kadhalika, Mwinyi anasema hali hiyo ilisababisha uhaba wa chakula na kwamba miaka ya 1984 hadi 1985, mazao yaliyokuwa yanapitia Shirika la Usagaji la Taifa (NMC), yalianza kupungua.

"Nilipata faraja kubwa pale Mwalimu Nyerere, wakati huo akiwa Mwenyekiti wa CCM, alipojitokeza wazi kuwatetea wafanyabiashara wadogo wanaosaidia wananchi kupata mahitaji yao muhimu...akasema wazi kuwapiga marufuku ni kuwakosesha njia halali ya kipato," anasema Mzee Mwinyi;

Mzee Mwinyi anabainisha kwamba: "Mwaka 1988 tukaruhusu wafanyabiashara kununua kutoka NMC, na kusafirisha huku na kule kuliko kuwapo na uhaba wa chakula na wananchi walikihitaji. Dhana ya ruksha ikazidi kushika kasi."

# Majaliwa ataka vyuo vitilie mkazo utafiti na ubunifu

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, ameviagiza vyuo vikuu nchini na taasisi mbalimbali kuwekeza nguvu katika kuendeleza utafiti, ubunifu ili zilete manufaa kwa taifa.

Alitoa rai hiyo jana kwenye maadhimisho ya wiki ya sita ya utafiti na ubunifu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, yaliyokuwa na kaulimbiu 'Utafiti na Ubunifu kwa Maendeleo Endelevu ya Viwanda na Jamii'.

Alisema serikali imedhamiria kujenga uchumi wa viwanda na itaongeza jitihada za uwezeshaji katika utafiti ili kujipanga katika mabadiliko yanayotokea katika jamii.

Majaliwa alisema utafiti na ubunifu ni suala lenye umuhimu katika taifa, kwa kuwa serikali haiwezi kufanya uamuzi wa kimaendeleo bila kufanya utafiti.

Aliwataka watafiti kuongeza kasi ili huduma zinazotolewa ziwe za kisasa na kuongeza tija katika uzalishaji.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema: "Tunahitaji mipango na mikakati yetu wenyewe kupiga hatua ya kimaendeleo na bila kuwa na utafiti juhudi zinazofanyika haziwezi kuzaa matunda".

Aliongeza kuwa katika kuhakikisha kuwa taifa linakwenda sambamba na mabadiliko ya kiteknolojia, ni lazima utafiti wa kimaendeleo utiliwe mkazo.



"Utafiti unasaidia kugundua kanuni na maarifa na kuweza kutengeneza nadharia muhimu za kielemu, pia utafiti unachangia mbinu katika kuleta maarifa na kuongeza hali ya kujifunza sambamba na kuchochea usomaji, kuwezesha kubaini fursa kama upatikanaji wa masoko katika bidhaa zinazozalishwa nchini," alisema Majaliwa.

Aidha, alitoa agizo kwa vyuo vikuu vyote kuweka utaratibu wa kufanya utafiti na ubunifu, pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kulipa kipaumbele suala hilo ili liweze kuwa na tija na manufaa kwa taifa.

"Nitoe maelekezo kwa vyuo vikuu vyote nchini kuweka utaratibu wa kufanya utafiti na kisha kuonyesha matokeo ya utafiti huo kama ilivyofanya UDSM, katika kufanya hivyo mtaimarisha uhusiano wa karibu baina ya vyuo na soko la ajira, lakini pia kunaweza kuwa moja ya sababu ya kuwavutia wafadhili na kupanua wigo wa ushirikiano wa ndani na nje ya nchi," alisema Majaliwa.

Waziri Mkuu Majaliwa alisema vyuo viweke bayana suala la kubiashanisha matokeo ya utafiti wake pamoja na kuandaa mikakati ya utekelezaji.

Alisema lengo kuu ni Tanzania ifike mahali utafiti uwe mkombozi wa maendeleo, kuacha mazoea ya kutunza matokeo na majarida katika makabati pindi zikikamilika.

"Watu wa viwanda ili kuunga mkono maendeleo ya utafiti za vyuo vikuu mnatakiwa mtoe ufadhili wa utafiti na bunifu badala ya kutegemea serikali."

Aidha, Waziri Mkuu Majaliwa aliwataka wakuu wa vyuo kuanzisha vitengo vya utafiti ili wananchi na wasomi walioko kwenye vyuo hivyo waweze kufanya.

"Tutenge eneo zaidi la kuonesha bidhaa zilizozalishwa kutokana na utafiti tulizozifanya. Kila mmoja atambue kuwa ubunifu ni nyenzo muhimu ya kutuwezesha kuhimili ushindani wa uchumi na kibiashara hapa nchini kwetu na duniani kwa ujumla."

## Ndugai amtambulisha Katibu mpya mwanamke bungeni

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amesema Bunge limepata mwanamke wa kwanza kuwa Katibu wa Bunge tangu lianzishwe mwaka 1926.

Ndugai aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akimtambulisha rasmi bungeni, Katibu Mpya wa Bunge, Nenelwa Mwihambi.

Mbali na kumtambulisha, Spika Ndugai alimpongeza katibu hiyo na kusisitiza kuwa wanawake wanaweza kuongoza na kuwataka wabunge kumpa ushirikiano.

"Naomba nimtambulishe kwenu katibu huyo mpya wa Bunge, kama mnavyofahamu Bunge lilianza zamani mwaka 1926 kwa hiyo bado miaka mitano au minne tutimize miaka 100."

Aliongeza, "huyo ndiyo mwanamke wa kwanza kuwa Katibu wa Bunge, hivyo tuna mpongeza naomba apewe ushirikiano kuonyesha wanawake wanaweza."

Katika hatua nyingine, Spika Ndugai aliwaapisha wabunge wawili wapya wa CCM ambao ni Mbunge wa Muhambwe, Dk. Florence Samizi na Mbunge wa Buhigwe, Kavejuru Felix.



# WFP yaipatia TASAF bil. 1.6/- usalama chakula




Mkurugenzi Mkazi wa WFP, Sarah Gordon-Gipson na Mkurugenzi Mkuu wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, wakitia saini makubaliano. **PICHA: WFP**

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Chakula (WFP) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wamesaini mkataba wa makubaliano wa Dola za Marekani 725,000 (sawa Sh. bilioni 1.6), kuongeza nguvu wa usalama wa chakula kwa kaya maskini 300,000.

Taarifa iliyotolewa na WFP kwa vyombo vya habari jana, ilisema Mkurugenzi Mkazi wa WFP nchini, Sarah Gordon-Gibson, alisema kuna haja ya kuongeza nguvu kwenye usalama wa chakula kuhakikisha kuna chakula cha kutosha na kuwafikia wenye uhitaji.

"Mpango wa kusaidia kaya maskini unahitajika kuhakikisha wanapata mahitaji muhimu yakiwamo ya chakula," alisema.

Pia alisema msaada huo utasaidia ushiriki wa kaya maskini kupanga mahitaji yao yakiwamo ya shule, vituo vya afya na huduma ya maji.

Katika makubaliano hayo WFP itasaidia kaya hizo kutumia teknolojia ya kidigitali kwa malipo mbalimbali na kuhifadhi data.

"Tunashukuru kwa msaada huu kutoka WFP ambao umekuja kwa wakati mwafaka tukiwa katika mpango wa kupanua wigo wa kuwafikia walengwa wetu," alisema Mkurugenzi Mkuu wa TASAF, Ladislaus Mwamanga.

Msaada huo kutoka WFP unatokana na michango kutoka kwa wafadhili mbalimbali wanaotoa misaada kwa shirika hilo kuwasaidia wenye uhitaji.

# RC asimulia Rais Samia alivyomkosesha usingizi

**Na Richard Makore,**

**MWANZA**

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Albert Chalamila, amekabidhiwa mikoba ya kuongoza mkoa huo, huku akisimulia alivyokosa usingizi kwa takribani miezi miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na wafanyakazi na viongozi mbalimbali wa Mkoa wa Mwanza baada ya kukabidhiwa ofisi na mtangulizi wake, ambaye kwa sasa ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela.

Aliwaambia wafanyakazi na viongozi hao kuwa katika kipindi hicho cha miezi miwili hakupata usingizi vizuri kwa kuwa hakujua hatima ya nafasi yake baada ya John Magufuli kufariki na kuingia Rais Samia.

"Nilikuwa nikilala naacha kiredio kinaongea kinapiga piga nyimbo, lakini nikisikia sauti ya Samia nashtuka usiku huo," alisema Chalamila.

Alisema katika kipindi hicho cha uongozi wa Rais Samia kwa miezi miwili alikuwa akilala vizuri, lakini akiamka asubuhi anakuwa kama anaumwa.

Akizungumzia mipango yake katika Mkoa wa Mwanza, Chalamila aliwataka watumishi wote kufanya kazi kwa bidii na kujiepusha kufanya hujuma kwa Rais Samia, ili aonekane ameshindwa kumudu majukumu yake.

"Lazima wote mfanye kazi kwa bidii kuanzia wenyeviti wa vitongoji hadi ngazi ya mkoa na mkishindwa kufanya hili itaonekana kama mnafanya hujuma kwa Rais Samia," alisema.

Aidha, aliwaomba wazee mkoani humo kumwazima busara kwa kuwa za kwake anaona hazitoshi ili aweze kutimiza majukumu yake.

"Wakati mwingine naomba wazee wangu mniongezee busara ninapokuwa nataka kutoa maamuzi naona hizi za kwangu kama hazitoshi," alisema Chalamila.

Kwa upande mwingine, Chalamila aliwataka wafanyabiashara kulipa kodi za serikali kwa hiari, huku akiwataka waliokabidhiwa jukumu la kukusanya kodi nao kufanya kazi yao bila kutumia nguvu.

Aliwataka wafanyabiashara kwa upande wao kuwa wepesi kulipa kodi huku akiwataka Wakurugenzi wa Halmashauri zote kuweka mkazo ili kufikia lengo la kukusanya Sh. bilioni 43 kwa mwaka ambayo ni mapato ya ndani.

Akizungumza muda mfupi kabla ya kumkabidhi ofisi, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongela, aliwashukuru waandishi wa habari kwa ushirikiano wao katika kipindi cha miaka mitano.

Aidha, aliwapongeza wananchi wa Mkoa wa Mwanza kwa namna walivyompa mawazo mazuri ya kujenga mkoa wao, huku akiwataka viongozi kuendelea kuwaheshimu badala ya kujiona wao wanajua kila kitu.

NMB
Karibu yako

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA 21 WA WANAHISA WA BENKI YA NMB ILIYOREKEBISHWA

**Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka wa wanahisa wa NMB utafanyika kwa njia ya mtandao saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa, Juni 4, 2021. Kampuni imerekebisha maazimio kwenye Taarifa ya Mkutano Mkuu na imeongeza ajenda nyingine. Kwasasa Ajenda itakuwa kama ifuatavyo:**

21.1 MATANGAZO NA AKIDI
21.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO
21.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 20 ULIOFANYIKA TAREHE 5 JUNI 2020
21.4 YATOKANAYO NA MKUTANO WA 20 WA WANAHISA
21.5 KUPOKEA, KUJADILI NA KUPITISHA RIPOTI YA WAKURUGENZI NA TAARIFA ZA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020
21.6 KUIDHINISHA GAWIO KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2020
21.7 KUPOKEA NA KUIDHINISHA MALIPO YA WAKURUGENZI
21.8 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA MABADILIKO KWENYE KANUNI ZA KAMPUNI
21.9 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA KUJIUDHURU NA KUTEULIWA KWA WAKURUGENZI WA BODI
21.10 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA UTEUZI WA WAKAGUZI WA HESABU KWA MWAKA UNAOMALIZIKA 31 DESEMBA 2021
21.11 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima atume kwa njia ya mtandao nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho chake au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni (kwa njia ya mkono au mtandao) kabla ya saa 4 asubuhi Alhamisi ya tarehe 3 Juni 2021.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atahudhuria kwa njia ya mtandao. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya NMB (www.nmbbank.co.tz).
4. Wakurugenzi wamependekeza ulipwaji wa gawio la shilingi 137 kwa kila hisa, inayoleta jumla ya shilingi 68.5 bilioni kutokana na faida ya mwaka 2020.

**Tarehe za kuzingatia:**

| | |
|---|---|
| **Tarehe ya tangazo:** | **14 Mei 2021** |
| **Hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **14 Mei 2021** |
| **Mwisho wa hisa kuuzwa pamoja na gawio :** | **2 Juni 2021** |
| **Hisa kuanza kuuzwa bila gawio:** | **3 Juni 2021 nakuendelea** |
| **Daftari la wanahisa kufungwa:** | **7 Juni 2021** |
| **Malipo ya gawio kwa wanahisa:** | **kuanzia tarehe 16 Juni 2021** |

Kwa amri ya Bodi ya Wakurugenzi,

Lilian R. Komwihangiro
Katibu wa Kampuni
7 Mei 2021

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu ya usalama ni bora kuliko makusanyo ya faini

UTII wa sheria zikiwamo za usalama barabarani bila shuruti ni hatua muhimu ambayo kwa kiasi kikubwa unapunguza ajali zikiwamo za kizembe ambazo kwa miaka mingi zimesababisha vifo, ulemavu, uharibifu wa miundombinu na vyombo vya usafiri.

Kutokana na ukweli huo, polisi na wadau kama Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji Ardhini (LATRA), wanatoa elimu kwa madereva na watumiaji wa barabara kuhusu umuhimu wa kuzingatia sheria.

Tunaamini wakati wa wiki ya nenda kwa usalama barabarani na kwenye majukwaa mengine wanafanya hivyo wakilenga kuwawezesha kila mmoja kutii sheria za usalama barabarani, miongozo na taratibu nyingine bila kulazimishwa au kushurutishwa, kwa ajili ya usalama wao, watumiaji wengine na vyombo.

Katika juhudi hizo za polisi, Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Simon Sirro, anasema ajali za barabarani kuanzia Januari hadi Aprili, mwaka huu zimepungua kwa asilimia 29.1 na kwamba yote hayo ni matokeo ya elimu kwa umma iliyosaidia kutii sheria za usalama barabarani bila kushurutishwa.

Anasema kuanzia Julai 2019 hadi kufikia Julai mwaka jana, Shilingi bilioni 56 zilikusanywa, lakini kiwango hicho kimepungua, ikiwa ni matokeo ya watu kutii sheria.

Hiyo ni habari njema, kwa kuwa kupungua kwa makusanyo ya faini ya makosa ya barabarani na ajali, ni wazi elimu hiyo imekuwa na tija kwa Watanzania, hivyo tunawapongeza polisi kwa juhudi hizo ambazo zinaokoa maisha ya watu, miundombinu na vyombo vya usafiri.

Ni ukweli makosa ya barabarani yamekuwa yakigharimu maisha ya watu kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo uzembe wa kutotii sheria, yakihusisha kupiga na kupokea simu barabarani, mwendo kasi, kupita magari mengine kwenye maeneo yanayokatazwa hasa kwenye milima, mabonde, kuendesha magari mabovu na kuingia barabarani bila mpangilio.

Uharibifu wa miundombinu hasa taa za barabarani, mabamba ya kingo za madaraja, alama za utambulisho wa maeneo mbalimbali kama vivuko vya wenda kwa miguu, kuwapo mteremko mkali, milima na makazi ya watu unashuhudiwa mara kwa mara na husababisha hasara kwa taifa na mtu mmoja mmoja.

Hivyo, zinapokuja taarifa za kupungua makusanyo ya faini na ajali, ni wazi kuwa polisi wanafanya kazi nzuri zinazofanikisha watumia barabara kuacha kupuuza sheria.

Mafanikio hayo ni tija kwa vile faini kubwa zilimaanisha uzembe na uvunjaji wa sheria ambayo kwa wengine walipoteza maisha, kupata ulemavu na barabara ziliharibika hiyo hatua iwe ni fursa kwa polisi kuendelea kutoa elimu kwa watumia barabara ili idadi ya wale wanaotii sheria bila shuruti izidi kuongezeka na kitisho kwa maisha ya watu kiondoke.


Tunaamini kiwango cha waliopata elimu ya usalama barabarani na kutii sheria bila shuruti kikiendelea kuongezeka, hatimaye hakutakuwa na faini tena, aidha ajali za kizembe zitaondoka na pengine hakutakuwa na vifo vingi, majeruhi, ulemavu, wakati miundombinu na vyombo vya usafiri vitabaki salama.

Tunaona kusimamia sheria zisivunjwe, ni jambo jema tena unaojikita zaidi katika kutoa elimu ya matumizi sahihi ya barabara, kwa kuwa yamekuwapo malalamiko ya kutozwa faini zaidi kuliko kuelimishwa.

Katika jamii, wapo baadhi ya watu ambao ni vigumu kubadilika hao ndio wasioweza kutii sheria bila shuruti, hao polisi iendelee 'kuwatibu' na kuwasaidia wakiwaelimisha, lakini hatua nyingine kama kuwatoza faini, kufungiwa leseni na kufikishwa mahakamani ziendelee ili wabadilike.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wizara iharakishe kiama 'tuma kwa namba hii'

Na Christina Mwakangale

KUKUA kwa teknolojia kumeleta matukio mbalimbali yakiwamo yenye manufaa lakini mengine yana athari hasi yote hayo yakiwagusa watumiaji wa huduma hizo wanaotumia kompyuta na simu.

Zama hizi simu za mkononi ndiyo kila kitu, zinafanikisha huduma za benki, taarifa muhimu za kielimu, kibiashara na uchumi, makazi ya watu, mitaa ni albamu ya picha na kwa wengine ni faragha kwa vile hutunza siri zao.

Kutokana na umuhimu huo kuna ongezeko la watumiaji wa laini za simu iliyofikia laini 53,063,085 hadi mwaka huu kutoka laini 48,939,530, imwaka jana, kwa mujibu wa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Faustine Ndugulile.

Idadi hiyo ni kubwa na inaendelea kuongezeka na suala la umiliki wa laini ya simu zaidi ya moja si geni nchini, pengine ni kutokana na kuwapo kwa kampuni kadhaa ambazo kila moja ina mfumo tofauti wa kutoa huduma na kuvuta wateja zaidi.

Hata hivyo, ili wingi wa laini hizo unaomaanisha idadi kubwa ya watumiaji uwe na tija elimu ya matumizi sahihi ya teknolojia hiyo ndiyo inayohitajika hasa kudhibiti baadhi ya watumiaji wanaotumia simu kuwaibia kimtandao wateja wengine.

Hivi karibuni Rais Samia Suluhu Hassan, alizungumzia kuhusu kuwapo kwa wizi wa mtandaoni, ambao wahusika wanatumia laini za simu za kampuni tofauti kutekeleza azma yao.

Kutokana na kukua kwa teknolojia, wahalifu hao nao huja na mbinu tofauti, hivi sasa hutuma ujumbe wa maandishi kwamba 'ahadi ya mchango wa harusi uliyotoa, itume kwenye namba hii...' Wapo wanaoamini na kutuma fedha, hivyo kuibiwa.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, hivi karibuni anasema serikali inaandaa utaratibu wa kuhakiki laini za simu nchini na zitakazobainika kutumika ndivyo sivyo zitafungiwa.

Uamuzi wa wizara umepokelewa kama njia bora ya kupambana na uhalifu mtandaoni ambao kwa sasa umeshika kasi nchini, hadi kufikia hatua ya kuwa moja ya mijadala bungeni.

Wabunge kadhaa bungeni walieleza jinsi walivyotapeliwa huku wakiiomba serikali kuchukua hatua. Waziri Ndugulile, anasema anataka kukumbukwa kama waziri aliyeleta mageuzi yaliyogusa maisha ya watu wengi, basi hili la kuibiwa kwenye mitandao liwe mojawapo kwa sababu wengi wanaathiriwa.

Anasema ni wakati wa kufanya mabadiliko makubwa ya sheria zinazosimamia sekta hiyo, akisisitiza kutolewa kwa elimu kuliko kukamata watu, akisema ame-

> **"Unamtoza kodi mtu karusha mtandaoni kazi yake ya ushereheshaji (MC) au wimbo wake, huku ni kuua kazi zao, tunataka tuondoke huko," anaisitiza na kuongeza kuwa maboresho ya sheria ya kulinda faragha ipo mbioni na lengo ni kuboresha na si kuminya uhuru wa watu kujieleza na kutumia mitandao, bali kulinda taarifa za watu kutotumika ovyo ikiwamo kusambazwa duniani.**

baini wengi hawana uelewa wa teknolojia. Pia, anasema wapo ambao hawajui sheria hivyo kutumia ovyo mitandao.

"Unamtoza kodi mtu karusha mtandaoni kazi yake ya ushereheshaji (MC) au wimbo wake, huku ni kuua kazi zao, tunataka tuondoke huko," anaisitiza na kuongeza kuwa maboresho ya sheria ya kulinda faragha ipo mbioni na lengo ni kuboresha na si kuminya uhuru wa watu kujieleza na kutumia mitandao, bali kulinda taarifa za watu kutotumika ovyo ikiwamo kusambazwa duniani. Akiwasilisha makadirio ya wizara yake, Waziri Ndugulile anasema, laini za simu zinazotumika zimeongezeka kutoka 48,939,530 mwaka 2020 hadi kufikia laini 53,063,085 mwezi Aprili mwaka huu sawa na ongezeko la asilimia 10.8.

Aidha, anasema watumiaji wa intaneti wameongezeka kutoka 26,832,089 mwaka 2020 hadi kufikia 29,071,817 mwezi Aprili mwaka huu sawa na ongezeko la asilimia 8.3.

Yote haya yanaonyesha ni kwa jinsi gani taifa linahitaji kuwa na udhibiti wa laini za simu ambazo pengine zimefanikisha kuibwa mamilioni ya fedha zilizotumwa kwa 'wajanja' baada ya kutuma ujumbe wa tutumie mchango wako wa harusi, kikoba, au fedha ulizokopa, ada ya shule kwenye namba hii.

HABARI KITAIFA

# Bandari 'bubu' 24 kurasimishwa

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limesema bandari bubu 24, zitaanza kurasimishwa kutokana na kufanya shughuli zake muda mrefu na huduma za usafirishaji.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Meli kutoka TASAC, Nelson Mlali, alisema ufukweni kumebainika bandari hizo zimekuwa zikitoa huduma ya kupakua, kusafirisha mizigo kama zingine.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki kwenye semina ya wanahabari kuwajengea uzoefu wa shughuli na huduma zinazotolewa na shirika hilo, ambalo husimamia vyombo vya usafiri wa majini katika baharini na ziwani.

Alisema zipo bandari bubu zipatazo 120 kwenye fukwe kadhaa nchini, akisema TASAC kama msimamizi wa shughuli za majini kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), wataanza kutoa vibali, leseni kwa bandari hizo, ili serikali ipate mapato.

"Bandari kavu zilipoanzishwa mwaka 2007/2008 na kutungiwa sheria mwaka 2016, ni baada ya msururu uliokuwapo bandarini. Pia ilikuwa kusaidia bandari kuu isisheheni mizigo kwa kuwa kuna shehena kubwa zinasubiri kuwasili kila siku," alisema Mlali.

Alibainisha kuwa mawakala wa usafirishaji mizigo waliopewa leseni na kutoa huduma ni 24, na kwamba uondoshaji mizigo bandarini hufanyika haraka, iwapo meli iliyoleta imelipia vibali vyote, ikiwamo huu kodi kwa wakati.

Ofisa Mahusiano ya Jamii TASAC, Nicholaus Kinyariri, alisema shirika linatekeleza majukumu mbalimbali yakiwamo usimamizi na udhibiti huduma za bandari na usafiri wa meli, biashara pamoja na kusimamia maslahi ya bidhaa za kipekee ikiwamo chakula, madini, silaha.

Kinyariri alibainisha kwamba tangu TASAC ianze kazi mwaka 2018, imetoa leseni 804 za uwakala wa meli kwa mwakala, kuboresha huduma za usafiri wa majini.

Pia aliema ili kuimarisha ulinzi, mapato shirika hushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Jeshi la Polisi-Kikosi cha Majini, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na Shirika la Kimataifa la shughuli za Majini (IMO).

Meneja Udhibiti wa huduma za Bandari. Julius Mitinje, alisema shirika hilo linafanya udhibiti katika maeneo ya pwani ya bandari za Dar es salaam, Tanga na Mtwara pia kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa.



Mkulima wa zao la ufuta, Hassan Abdallah, akivuna zao hilo katika moja ya mashamba darasa katika kata ya Nampiluka, Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi jana. **PICHA: ABDALLAH HAMISI**

# Serikali yatakiwa kutilia mkazo sekta ya uvuvi

**Na Frank Kaundula, MOROGORO**

WADAU wa maendeleo sekta ya uvuvi nchini wameiomba serikali kuweka mkazo na mpango mkakati ili kuinua sekta hiyo ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika kukuza pato la taifa kila mwaka.

Wakizungumza za Nipashe, wadau hao akiwamo, Peter Sumun alisema licha ya Watanzania wengi kujihusisha na uvuni lakini bado sekta hiyo haina tija kwenye pato la taifa kitendo ambacho hakina afya.

"Mbali na kwamba Watanzania wengi wanajishughulisha na uvuvi lakini sekta hii inachangia asilimia 1.71 ya pato la taifa jambo ambalo siyo zuri, hivyo tunaiomba serikali kulitazama hili kwa jicho la tatu ili kuongeza tija zaidi," alisema Sumun.

Alisema kuwa sekta hiyo ni muhimu kwani mbali na kuwapatia wananchi kipato cha kujikimu pia serikali hupata mapato kutokana na ushuru unaokusanywa.

Hivyo, aliomba kuboreshwa kwa mazingira yanayoendesha shughuli zote za uvuvi nchini vinginenyo bado sekta hiyo haitakuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa pato la taifa.

Mhadhiri Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Paul Onyango, alieleza kuwa kitendo cha kutokusanya mapato yatokanayo na uvuvi kutokuwa sahihi kunaweza kuathiri takwimu zitokanazo na sekta hiyo muhimu.

Onyango alisema kuwa sekta ya uvuvi ni moja ya sekta muhimu hapa nchini inayoweza kuliingizia taifa fedha nyingi, hivyo serikali haina budi kuhakikisha inatatua changamoto zilizoikabili sekta hiyo ikiwamo kutokomeza uvuvi haramu.

Ofisa kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Yusufu Semguruka, alieleza umuhimu wa uboreshaji wa sekta hiyo ili ilete tija kwa taifa.

Alisema uboreshaji wa sekta hiyo utasaidia kukuza pato la taifa ikiwamo kuhakikisha takwimu katika mazao ya maziwa, mito na bahari zinakusanywa kikamilifu, kwamba kutaonyesha dira katika sekta hiyo. Aidha, alisema serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa uvuvi nchini ili kuhakikisha sekta hiyo inakuwa na tija kwa taifa, lakini wananchi hususani wavuvi nao wananufaika zaidi kiuchumi kutokana na shughuli zao hizo za kila siku.

# TBS yaridhishwa uzalishaji vifungashio

**Na Mwandishi Wetu, MWANZA**

MAOFISA wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), wamefanya ukaguzi katika viwanda vinavyozalisha vifungasho na usajili wa majengo ya bidhaa za vyakula na vipodozi mkoani Mwanza, huku wakielezea kuridhishwa na mwitikio wa wananchi katika kutumia bidhaa zilizosajiliwa na kuthibitishwa ubora na shirika hilo.

Miongoni mwa bidhaa za vifungashio na vibebeo vilivyokaguliwa ni pamoja na mifuko ya plastiki ya kufungia mikate, maziwa, barafu na karanga.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, Mkaguzi wa TBS, Hellen Mamkwe, alisema bidhaa hizo zinasajiliwa na TBS ikiwa ni kutekelezwa takwa mojawapo la Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kuhusiana na vifungashio vya plastiki.

Alisema mtengenezaji ya vifungashio anatakiwa aweke anwani ya kiwanda chake, aoneshe kwamba ni kwa ajili ya kufungashia bidhaa za chakula na bidhaa hiyo inaweza kurejereshwa.

Alisema takwa jingine muhimu hi bidhaa hiyo ioneshe kuwa imesajiliwa na kuthibitishwa ubora wake na TBS.

Alisema wanachokifanya jijini Mwanza ni kuhakikisha wanawatambua wazalishaji wote wa bidhaa za vifungashio kwa kupita kwenye viwanda mbalimbali vinavyojiusisha na uzalishaji wa bidhaa hizo ili kujua ni vifungashio vya aina gani wanavyozalisha katika viwanda vyao.

Alisema wazalishaji wengi wamethibitisha ubora wa bidhaa zao TBS. Kwa upande wa usajili wa majengo ya bidhaa za vyakula na vipodozi, Mamkwe alisema wamefanyakazi hiyo Wilaya ya Ilemela na Nyamagana, bado kazi hiyo inaendelea.

Alisema katika Wilaya ya Nyamagana wameanza na eneo la Mkuyuni na Kata ya Butimba na kwamba zoezi hilo limekuwa na mwitikio mzuri. Kuhusu mwitikio wa wananchi kuuza bidhaa zilizothibitishwa na TBS, alisema ni mzuri.

Alitoa mwito wa wananchi wanapoenda kununua bidhaa wahakikishe wanaangalia tarehe ya mwisho ya matumizi kama haina haipo wasinunue bidhaa hiyo.

Kwa upande wake Ofisa Usalama wa Chakula wa TBS, Deus Mlenga, alisema kwa sasa kiwango cha uelewa ndani ya jamii kuhusiana na matumizi ya bidhaa zilizosajiliwa na kuthibitishwa na TBS ni mkubwa.


JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER.

DALALI WA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA – MWANZA,GEITA,BUKOBA,MUSOMA,
DEBT COLLECTIONS & AUCTIONEERING
*HEAD OFFICE –Buzuruga plaza 2nd Floor Room No. 207 Mwanza*
*P.O BOX 11126 MWANZA, 0713/0789/0768-203040*
josinacompany@gmail.com,josinacoltd@gmail.com

TANGAZO TANGAZO TANGAZO

*JOSINA COMPANY LIMITED ITAENDESHA MNADA WA HADHARA WA KUUZA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WA **LETSHEGO BANK TANZANIA LIMITED** KUANZIA **26/05/2021 HADI 01/06/2021** MUDA NI KUANZIA SAANNE ASUBUHI NA KUENDELEA*

| NA | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | MOHAMED AMANI RAMADHAN | PLOT NO.109 Block A Mhandu PLOT NO.3Block HDR Igogo PLOT NO.1ABlockAIX Kirumba | MHANDU IGOGO KIRUMBA | 26/5/2021-01/06/2021 | JOSINA CO LTD |
| 2. | JOHN BHOKE GENTEGAI | PLOT NO.1475 Block A Luchelele | LUCHELELE | 26/5/2021-01/06/2021 | JOSINA CO LTD |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. DHAMANA ZITAUZWA KAMA ZILIVYO, MNUNUZI ATALIPIA 25% YA BEI YA MNADA. 75% ITALIPWA NDANI YA SIKU 14 KUTOKA SIKU YA MNADA. AKISHINDWA KULIPA, MALIPO YA AWALI HAYATARUDISHWA.
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI ZA UMILIKI ZITAKUWA JUU YA MNUNUZI.
3. UKAGUZI WA DHAMANA ZINAZOUZWA UTAANZA SIKU MOJA KABLA YA MNADA NA GHARAMA ZA KUMPELEKA MTEJA KWENYE DHAMANA ZITAKUWA JUU YA MTEJA.

KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-
MKURUGENZI Josina Co. Ltd: 0768 203 040, WHATSAPP NO: 0713 203 040



Mtaalamu anayehusika na malighafi zinazotumika kutengeneza bia (material clerk) wa SBL, Deogratius Adam (kushoto), akiwaelezea wanafunzi wa Chuo cha Kilimo na Mifugo Kilacha hatua mbalimbali ambazo hupitiwa wakati wa utengenezaji wa bia wakati wanafunzi hao, walipotembelea kiwanda cha SBL kilichoko Moshi mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. Wanafunzi hao ni wanufaika na mpango wa ufadhili wa masomo unaojulikana kama Kilimo Viwanda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bunge lataka uwazi ajira za walimu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limesema linataka uwazi katika utoaji wa ajira za walimu huku likielekeza kamati zake kufuatilia kwa karibu walioajiriwa.

Spika wa Bunge, Job Ndugai aliyasema hayo jana baada ya kumalizika kwa kipindi cha maswali na majibu bungeni.

Hivi karibuni, serikali ilitoa kibali cha ajira za watumishi wa kada mbalimbali za afya ni 2,726 na walimu ni 6,949 wa shule za msingi na sekondari na hadi juzi zaidi ya watu 120,000 walikuwa wameomba ajira hizo.

Akizungumza bungeni, Spika Ndugai alisema kuna ajira 8,000 za walimu zilitangazwa, lakini kamati za bunge husika hazikufuatilia kwa karibu, katika hizo 6,000 bunge litafuatilia kindakindaki na mfumo wake uwe wa wazi na wakueleweka.

Alizitaka Kamati za Bunge zinazohusika zijitahidi kuwa macho na mambo ya kitaifa katika ufuatiliaji wake na si kusubiri Spika peke yake awaambie cha kufanya.

Alisema ajira hizo zikikamilika kamati husika itoe taarifa zoezi liliendaje ili wajiridhishe na kuishauri serikali kama kuna maeneo ya kurekebisha.

"Kamati zetu zifanye kazi mjitahidi sana kufanya kazi zenu ambazo mnahusika, hasa zile kamati za kisekta msikae tu fuatilieni mambo nyie ndio bunge, msiache tu mambo yakawa yanaenda tu... Mtakumbuka kipindi kilichopita kulikuwa na ajira za walimu 8,000 wangapi mnajua wapigakura wenu wamepata nafasi?"

"Mnawezaje kuwa na hakika mchakato wa wakati huo umekwenda unavyopaswa, ni kazi ya bunge kufuatilia kuwaita njooni tuelezeni tupe majina wapi ametoka ni kazi yenu."

"Kama sio kazi yenu ni kazi ya nani? Mnasubiri Spika awaambie kamati husika? Nyie mnaniambia kwamba mnataka tuwaite hawa kwa ajili ya kupata taarifa hii, nyinyi ndio kwa niaba ya wananchi."

"Tusipoangalia tutajikuta nchi hii baada ya kuwa na utumishi wa umma wa Watanzania wote tukawa na utumishi wa umma wa baadhi ya watu katika nchi hii."

"Hatuwezi kwenda hivyo sisi tuna wajibu wa ziada wa kuhakikisha sio tu ajira ngapi ngapi elfu ngapi zimeenda wapi kivipi," alisisitiza.

"Safari hii tuna ajira nadhani 6,270 kitu kama hicho hizo, 8,000 tusifuatilie kwa sababu limeshapita, lakini hizi 6,000 tuwaambie kabisa serikali tutazifuatilia kindakindaki na mfumo wake uwe na uwazi, unaoeleweka, uwe ambao hauna mambo mengine na ni vizuri kuja na fomula huku tunakoenda ambazo ni inclusive."

"Hata kama ni walimu basi wawepo Wamasai, Wamakonde, Wahaya, Wagogo, Waha, tunataka mfumo ambao ni inclusive tuingize watu wa aina mbalimbali katika nchi," alisema.

Alisema kuwapo na mfumo wa utumishi ambao unatoa sura ya nchi ilivyo.

# Mashine ya tani 70 yatumbukia bandarini

**Na Christina Mwakangale**

KATIKA hali isiyo ya kawaida mashine ya kunyanyua vitu vizito yenye uzito wa tani 70 imetumbukia baharini kwenye Bandari ya Dar es Salaam juzi, wakati ikishushwa kutoka kwenye meli.

Taarifa iliyotolewa jana na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), ilisema mashine hiyo ilizama katika eneo la gati ya Malindi, bandarini majira ya mchana.

Hata hivyo, hadi kufikia jana mchana TPA ilieleza kuwa juhudi za kuiondoa mashine hiyo ilikuwa inaendelea.

Akizungumza jana na Nipashe kuhusu tukio hilo, Meneja Uhusiano na Mawasiliano TPA, Nicodemus Mushi, alisema uopoaji wa mashine hiyo ulianza tangu jana kwa kutumia vifaa maalumu na wazamiaji.

Mushi alisema; "Tuna uwezo wa kuiopoa crane hii yenye uzito wa tani 70, vifaa vyetu vina uwezo wa kuopoa hata mzigo wa tani 100, tunazo mashine za kubeba vitu vizito 'gottwald cranes', iwapo kitu kizito kikizama baharini.

"Crane ilizama wakati ikishushwa na kutumbukia baharini, mashine hiyo ni mzigo wa mteja na meli pia si ya kwetu," alisema Mushi.

Kwa mujibu wa taarifa ya TPA, ajali hiyo haikusababisha madhara yoyote kwa watu huku ikiwaondoa hofu wateja wake.

Mamlaka hiyo ilisema, majira ya saa nane mchana mashine hiyo iliyokuwa kwenye meli ya LCT AJE 1, iliyowasili Dar es Salaam kupitia visiwa vya Songosongo, ilipata ajali na kutumbukia baharini.

# Kilimo chapigiwa chapuo ongezeko bajeti

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji, imetoa mapendekezo manane kwa serikali kufikia lengo la mapinduzi ya kilimo chenye tija nchini.

Akiwasilisha mapendekezo hayo jana bungeni, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Athuman Maige, alisema ni lazima serikali iimarishe bajeti ya sekta ya kilimo kutokana na mchango wake katika Pato la Taifa, ajira kwa wananchi na malighafi kwa ajili ya viwanda.

Alisema licha ya umuhimu huo bado serikali haijawekeza ipasavyo kuimarisha ukuaji wa sekta ya kilimo kwa kuwa kwa mwaka 2021/2022 imetengewa bajeti chini ya asilimia moja ambayo ni sawa na asilimia 0.08 ya bajeti kuu.

Alisema mengine ni kuwawezesha maofisa ugani kutekeleza majukumu yao na kuitaka kuajiri ili kukidhi mahitaji ikiwa ni pamoja na kuwatengea rasilimali fedha, kuwapatia vitendea kazi na kuwapa mafunzo ya mara kwa mara ya kuwaimarisha kufanya kilimo cha kisasa.

"Serikali iangalie uwezekano wa kutunga sheria itakayozitaka halmashauri kurudisha sehemu ya tozo zitokanazo na mazao ya kilimo kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo tofauti na hali ilivyo sasa ambapo maamuzi hayo hayajawekewa masharti ya kisheria na yanategemea utashi wa Mkurugenzi na Baraza la Madiwani," alisema Maige.

Jingine ni kuimarisha utafiti na uzalishaji mbegu na kutaka iendane na utafiti ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kutosha kwa ASA ili kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mazao.

Alisema kamati inashuari nguvu kubwa ielekezwe kwenye uzalishaji wa mbegu za mafuta ya alizeti, mchikichi na ngano ili kupunguza gharama kubwa ya fedha za kigeni inayotumika kuagiza bidhaa hizo nje ya nchi.

Aidha, kurejesha mfuko wa kuendeleza tasnia ya korosho, ambao umekuwa ukishuka kwa miaka mitatu mfululizo, kukabiliana na changamoto ya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa kwa kujenga vihenge na maghala ya kuhifadhia mazao, chanzo kikiwa ni miundombinu mibovu ya barabara na kutaka TARURA kupewa fedha za kutosha.

Jingine ni namna bora ya kuwezesha wakulima wadogo kupata mikopo yenye riba nafuu na kwamba ni muhimu ukawekwa utaratibu mahususi kuwezesha upatikanaji wa mikopo rafiki kwa sekta ya kilimo.

Pia, kuimarisha utengaji bajeti ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwa kuwa eneo la umwagiliaji linalofaa kwa kilimo ni hekta milioni 29.4 na kwa kuwa ufinyu wa bajeti umesababisha kutumia eneo linalofaa kwa umwagilaji kwa asilimia mbili.

Maige alisema kuimarisha ushirika nchini kwa kuelimisha wakulima umuhimu wa kujiunga kwenye ushirika, kuboresha uongozi, kudhibiti wizi na ubadhirifu ndani ya vyama na vifuate sheria.

HABARI KITAIFA

# Mzumbe chajivunia kupika viongozi akiwamo Samia

**Na Joseph Mwendapole,** ALIYEKUWA MOROGORO

CHUO Kikuu cha Mzumbe mkoani Morogoro, kinajivunia kuwa chimbuko la viongozi wengi mashuhuri akiwamo Rais wa awamu ya sita, Samia Suluhu Hassan.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Lughano Kusiluka, alisema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wanachama wa Jukwaa la Wahariri (TEF), walipotembelea chuo hicho.

Alisema chuo hicho ni cha nne kuanzishwa kikitanguliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo Kikuu Huria (OUT) na Chuo Kikuu cha Kilimo SUA, na kwamba kimepika viongozi wengi wa kitaifa.

Profesa Kusiluka alisema Rais Samia alisoma chuoni hapo mwishoni mwa miaka ya 80 na alisomea utawala wa umma, ambacho kilianzishwa kama chuo cha kimkakati katika mafunzo ya uongozi na utawala.

Aliwataja viongozi wengine mashuhuri waliosoma chuoni hapo kuwa ni Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, Naibu wake Christina Mndeme na aliyekuwa Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali, Ludovick Utouh.

Aliwataja wengine kuwa ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulah, Spika wa Bunge mstaafu, Anne Makinda, Katibu Mkuu Kiongozi Ombeni Sefue na wakuu wa mikoa mbalimbali ikiwamo ya Dar es Salaam, Pwani na Dodoma.

Alisemwa kwa mwaka wa masomo 2020/2021, chuo kimesajili jumla ya wanafunzi 12,343 wanaume ni 6,533 na wanawake ni 5,810 na kwasasa kinatoa mafunzo ya muda mrefu katika programu 31.

Alizitaja kuwa ni Shahada za Kwanza ikiwa ni pamoja na 25 zinazoendeshwa katika Kampasi ya Morogoro, nne katika Ndaki ya Mbeya na mbili katika Ndaki ya Dar es Salaam maeneo ya Tegeta.

Profesa Kusiluka alisema chuo hicho pia kinaendesha programu saba katika ngazi ya stashada na tisa katika ngazi ya astashahada pamoja na shahada za awali.

Alisema pia chuo kinaendesha mafunzo katika ngazi ya Shahada za Umahili (Masters) ikiwa ni pamoja na programu 20 katika kampasi kuu, programu sita katika Ndaki ya Dar es Salaam na programu moja katika Ndaki ya Mbeya.



Aliyekuwa mgombea urais kupitia CHADEMA, Lazaro Nyalandu (kushoto), akiangalia burudani iliyokuwa ikitolewa na kikundi cha ngoma cha Mbalamwezi (hakipo pichani). **PICHA: JUMBE ISMAILLY**

# UVCCM Singida wampokea Nyalandu

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MWENYEKITI wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Kheri James, amewataka wanachama wa chama hicho kukijenga katika ngazi zote ili kiweze kuwavutia wanachama wa vyama vingine kujiunga.

Kheri ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM Taifa, aliyasema hayo mjini hapa kwenye hafla ya kumpokea aliyekuwa mgombea wa nafasi ya urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) mwaka 2020, Lazaro Nyalandu, pamoja na wanachama wa vyama vingine baada ya kutangaza kuvihama vyama vyao na kujiunga na CCM.

Akiwasilisha salamu za Makamu Mwenyekiti wa CCM Tanzania Bara, Philip Mangula, Mwenyekiti huyo alisisitiza kwamba CCM kimesajiliwa sawa na vyama vingine, kina hadhi sawa na vyama vingine, ushawishi, lakini lazima kiwe na namna yake ya kujipambanua na kujitofautisha na vyama vingine.

Akitangaza kukihama CHADEMA, Nyalandu alisema;

"Ningeomba CCM ninayoirudia nyumbani watu waamke tena, fikra zetu ziamke tena, utashi wetu ufufuke, kwa mema mapenzi ya CCM ya kushirikiana katika shughuli mbalimbali kama vile kuoa twende, amefiwa twende, kusengenya sengenyana ile iliyokuwapo tuache, dhambi zile ndogo ndogo tuache na wale niliowakwaza naomba mnisamehe," alisema.

Nyalandu ambaye aliwahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Kaskazini, aliahidi kuzunguka katika wilaya kadhaa kufufua CCM iliyokuwa na utamaduni wa kushirikiana kwenye shida na raha.

Naye Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Lindi, Suleimani Mathew, alisema kabla ya kujiunga na chama hicho aliwahi kushika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya CCM, ikiwamo udiwani wa kata ya Vijibweni, Dar es Salaam.

# YPC yashauri vijana kutumia fursa usindikaji kujiajiri

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKURUGENZI wa Asasi ya Maendeleo ya Vijana (YPC), Israel Ilunde, amesema sekta ya usindikaji inatakiwa kuwekewa nguvu ya ziada ili vijana waweze kujiajiri.

Ilunde aliyasema hayo jana wakati wa kongamano la vijana lililoandaliwa na asasi hiyo, mjini Kibaha.

Alisema sekta ya usindikaji endapo itapewa kipaumbele itakuwa moja ya fursa za ajira kwa vijana kujiajiri.

ilunde alisema kilimo kina wigo mpana kwa kuwa kuna mkulima na mfanyabiashara ambaye ananunua mazao hayo na kuyauza na kupitia mazao hayo yanaweza kusindikwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi na kumfanya kijana achangamkie fursa ya kujiajiri.

Mratibu wa miradi wa YPC, Fred Mtei, alisema tatizo la ajira linaweza kupungua endapo sekta ya usindikaji itapewa kipaumbele.

Mtei alisema endapo vijana watapata mafunzo ya usindikaji watajiajiri na kusindika mazao ambayo yatakuwa yanaongezeka thamani na kuyauza maeneo mbalimbali.

Mshiriki wa kongamano hilo, Sara Mwakabinga, alisema vijana wanatakiwa kutambua kuwa kilimo si lazima kushika jembe, lakini wanaweza kuchukua fursa zilizopo kwa kuchukua mazao kuyasindika na kuyauza katika masoko mbalimbali.

Vijana pia walipendekeza kilimo kupewa umuhimu unaostahili na sekta ya usindikaji itambuliwe kama sekta mama na wanaoanzisha kampuni sekta ya kusindika vyakula waungwe mkono.

**Ilunde alisema kilimo kina wigo mpana kwa kuwa kuna mkulima na mfanyabiashara ambaye ananunua mazao hayo na kuyauza na kupitia mazao hayo yanaweza kusindikwa na kuuzwa ndani na nje ya nchi na kumfanya kijana achangamkie fursa ya kujiajiri**

# Spika Ndugai aipa ushauri Wizara Mifugo

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, ameshauri Wizara ya Mifugo na Uvuvi kubaki katika masuala ya utafiti na si kushughulika na mashamba ya kufuga mifugo.

Aidha, amesema Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO), imeshindwa kufanya kazi kwa ufanisi tangu mwaka 1967 na kushauri ibinafsishwe.

Ushauri huo aliutoa bungeni jana baada ya Naibu Waziri wa wizara hiyo, Abdallah Ulega, kujibu maswali ya Mbunge wa Makete (CCM), Festo Sanga.

Spika Ndugai alisema; "Yaani serikali inachunga ng'ombe na ranchi kitu ambacho Msukuma anaweza, Mgogo anaweza, serikali ifanye mambo ya maana ya serikali haya mashamba sijui Kongwa ranchi au kina nani tuwaachie wananchi washughulike nayo."

Alishauri serikali ibaki na masuala ya utafiti na si kuchunga ng'ombe.

"Wizara ya Mifugo tuangalie haya mambo tubadilike tutoke huko...miradi mingine bwana, mradi ambao yanaagizwa madume matano ya ng'ombe, wafanyakazi kibao wana madeni wanadai," alisema na kuongeza.

"Tunasubiri bajeti yetu ije tuone, lakini NARCO imeshindwa tangu mwaka 1967 ilipotaifishwa hayo mashamba hadi leo hamna kitu mnadhani nyie ndio mtaweza? Binafsisheni hiyo peke yake ndio njia ya kwenda."

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji ni mkakati gani wa serikali wa kuendeleza shamba la mifugo la Kitulo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ulega alisema shamba hilo ni miongoni mwa mashamba matano ya serikali ya kuzalisha mifugo na ni shamba pekee linalozalisha ng'ombe aina ya Freisian halisi.

"Mkakati uliopo ni wa miaka mitatu (2020/2021 - 2022/2023) ambao umelenga kuendeleza shamba kwa kuongeza ng'ombe wazazi kutoka 350 hadi 700, kununua madume ya ng'ombe wazazi 20, kuboresha malisho kwa kupanda malisho eneo la hekta 150, kuimarisha huduma ya uhimilishaji kufikia uhimilisha wa ng'ombe 300 kwa mwaka," alisema.

Alisema katika kutekeleza mkakati huo wizara kupitia bajeti ya mwaka 2021/22, imenunua madume matano ya ng'ombe wazazi kutoka shamba la Shafa lililopo mkoani Iringa, kilo 400 za mbegu za malisho kutoka Marekani na kilo 100 kutoka Kenya kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa malisho.

Vile vile, alisema shughuli nyingine ni uhimilishaji na ng'ombe 135 wamehimilishwa, ununuzi wa tangi la kupoozea maziwa lenye ujazo wa lita 3,000 na utaratibu wa ununuzi unakamilishwa.

"Shamba la Kitulo linahitaji uwekezaji wa kiasi cha Sh. bilioni 6.6 ili kufikia kiwango cha juu cha uzalishaji," alisema.

Alisema uwekezaji huo utaendelea kufanywa na serikali kadri ya upatikanaji wa fedha kwa kushirikiana na wadau wengine wa maendeleo.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akimwapisha Mbunge mpya wa Jimbo la Mhambwe (CCM), Dk. Florance Samizi, bungeni kwenye kikao cha 35 Bunge la 12 kilichofanyika jijini Dodoma jana. Mbunge huyo amechukua nafasi ya Dk. Philip Mpango aliyeteuliwa kuwa Makamu wa Rais.
**PICHA: IBRAHIM JOSPEH**

# Wataalamu kufanya uchambuzi vikwazo miradi

SERIKALI imeunda timu ya wataalamu ili kufanya uchambuzi wa kina kuhusu vikwazo katika miradi ya masoko ya kimataifa ya Murongo na Nkwenda ili kutoa mapendekezo ya namna bora ya kukamilisha ujenzi wake.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2021/22, serikali imetenga Sh. milioni 500 kwa ajili ya tathmini na uendelezaji wa masoko ya kimkakati ya mipakani.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Anatropia Theonest.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itamalizia ujenzi wa masoko ya kimataifa ya kitega uchumi ya Murongo na Nkwenda ili kuongeza chachu ya maendeleo ya Wilaya ya Kyerwa, mkoani Kagera.

Akijibu swali hilo, Kigahe alisema serikali inatambua umuhimu wa kuwa na masoko ya kimataifa ya kimkakati kwa ajili ya kukuza biashara na mauzo nje ya nchi kwa maendeleo na ustawi wa wananchi wake.

"Kutokana na umuhimu huo, serikali imechukua hatua mbalimbali za kuhakikisha masoko ya kimkakati hususan ya mipakani yanaanzishwa, kuboreshwa na kuendelezwa," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa mpaka kati ya Tanzania na Uganda, serikali iliamua kuanzisha masoko ya kimkakati ya kimataifa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa masoko ya Nkwenda na Murongo chini ya Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo wilayani (DASIP) uliokuwa unafadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

"Masoko hayo bado hayajakamilika kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo za ufinyu wa bajeti," alisema.

Alisema kazi ya tathmini na uendelezaji wa masoko ya kimkakati ya mipakani itafanywa kwa pamoja kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Kilimo.

Alisisitiza serikali inaendelea kushirikiana na wadau wengine kutafuta fedha za kukamilisha ujenzi wa masoko ya Murongo na Nkwenda kwa wakati.

## Sumbawanga yatengewa bil. 2.76/- miradi ya maji

WIZARA ya Maji imesema katika mwaka wa fedha 2021/22, imetenga Sh. billioni 2.76 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 18 ya maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga.

Hata hivyo, serikali itatoa fedha kwa kuzingatia miongozo ya kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi iliyopangwa katika bajeti husika.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kwela (CCM), Deus Sangu.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kusambaza maji kutoka skimu ya maji kata za Miangalua na Mnokola, Jimbo la Kwela.

Pia alihoji ni lini serikali itapeleka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi katika maeneo hayo.

Akijibu swali hilo, alihoji hali ya upatikanaji wa maji katika Kata za Miangalua na Mnokola ni asilimia 51.2.

"Kata hizi ya Miangalua inapata huduma ya majisafi kupitia mradi wa maji wa skimu ya Miangalua na visima virefu vinavyohudumia vijiji vya Miangalua, Tunko, Movu, Kavifuti na Nampako vya Kata hiyo na kijiji cha Mnokola kilichopo katika kata ya Mnokola," alisema.

Alisema katika kuhakikisha hali ya upatikanaji wa maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga inazidi kuimarika, serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji na kwa mwaka wa fedha 2020/21, miradi mitano ya maji imetekelezwa na kukamilika katika vijiji vya Nankanga na Sakalilo (kata ya Ilemba), Milepa na Kisa (kata ya Milepa), Kizungu (kata ya Muze) na miradi minne ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji katika kata za Mtowisa, Ikozi, Msandamuungano na Mufinga.



Nipashe
# TESA
Jumanne Mei 25, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

## Taasisi yataja ulipo uwezeshaji endelevu kwa kaya maskini



Ukurasa 12

## Wanaowahudumia wenye ulemavu wanasema haya...

ELIMU

**NA NIMI MWETA**

HELSB NI MZIGO

# Vinahitajika vyanzo, vigezo ushahidi mujarabu kuifuta



Shughuli za mahafali katika moja ya vyuo vya elimu ya juu. **PICHA: MTANDAO.**

'SHUGHULI za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) hazina ufanisi kwani gharama za uendeshaji wake na mapungufu yanayoambatana nayo yanazidi faida za uwepo wa chombo hicho na anadhani njia pekee ni kuifuta.'

Ni maoni ya aliyekuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ludovick Utouh.

Anayaeleza hayo kwenye jukwaa moja lililokuwa linajadili ripoti ya mwaka 2020 ya CAG iliyotolewa kuelekea mwisho wa mwezi Machi mwaka huu na kuzua mijadala maridhawa hasa bungeni. Lakini katika mahojiano na gazeti hili.

Katika kuitafakari kauli ya Utouh pengine maswali kadhaa yanaibuka mfano, elimu ya vyuo vikuu bila mikopo inawezekana au ni lazima wanafunzi wakopeshwe ili kuendelea na masomo ya elimu ya juu? Ni jambo gani linaweza kufanyika ili kuwepo na taasisi ya kusimamia mikopo hiyo?

Pengine, siyo rahisi kusema kuwa hisia hiyo ya CAG ni rahisi kukubaliwa kila mahali au miongoni mwa wataalamu kwa jumla, kwani mambo yanabadilika kulingana na wakati uliopo. Anachosema Utouh kilikuwa 'kweli' zaidi katika kipindi alichokuwa akiondoka madarakani au kuelekea mwisho wa awamu ya nne, na miaka michache iliyofuata. Hii ndiyo picha inayojitokeza katika kuangalia baadhi ya taarifa pembuzi za wakati huo, kwa mfano mojawapo ilichapishwa Septemba 4, 2016, ikisema kuwa vyuo vikuu vya Tanzania vina tatizo kubwa la mikopo kwa wanafunzi hewa, ambalo serikali ya awamu ya tano ililivalia njuga na kuelekea kulimaliza.

Wakati huo, serikali ilisimamisha mikopo ya wanafunzi takribani 2,000 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.2 baada ya zoezi la kuyakinisha utolewaji wa mikopo kubaini kuwa baadhii ya wanafunzi waliopewa fedha hizo walikuwa hewa. Kwa vile idadi ya wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu inazidi 100,000 uwepo wa mikopo 2,000 yenye hitilafu inaweza kuonekana ni jambo dogo, lakini fedha za mikopo zinafujwa, kwa kudhamiria au kutokana na uongozi hafifu, hivyo kuathiri mfumo mzima wa elimu ya juu na mwishowe, taifa linalotoa fedha hizo. Kimsingi ndicho alichoainisha CAG katika mada yake.

Ila kwa nyakati tofauti kumekuwa na taarifa njema zaidi kuhusu uhai na ufanisi wa mpango wa mikopo ya elimu ya juu na urudishwaji wake, ukiangalia taarifa iliyochapishwa Machi 21, 2019 mitandaoni na mashirika ya habari ya kimataifa, yakinukuu habari za hapa nchini. Taarifa hiyo iligusia kuongezeka kwa haraka kwa ufanisi katika miezi kadhaa iliyotangulia kwa suala la ukusanyaji malipo kwa wafaidika wa mikopo ya elimu ya juu, ambako kiasi cha wanafunzi 5,000 wapya wangepata mikopo katika mwaka huo wa fedha kutokana na kasi ya urudishaji. Moja ya sababu ni makato zaidi katika mishahara ya wafaidika.

Ukisikiliza alichosema Utouh na kilichojiri hivi karibuni wakati Rais Samia Suluhu Hassan, anachukua uongozi wa taifa kwa mfano katika hotuba yake ya Mei Mosi, kinachoonekana ni kuwapo mgongano wa hisia na mapendekezo nini kifanyike katika eneo hilo. Utouh anaonekana kukata tamaa kuhusu kuleta ufanisi katika eneo hilo, kwa msingi ule ule alioeleza kuhusu maeneo mengine ambako bodi hazifanyi kazi. Itakumbukwa kuwa Rais Samia aliagiza bodi za wafanyakazi ambazo pia zinahusika kuangalia maslahi ziundwe katika sekta tofauti au zianze kufanya kazi, ila kwa vile mishahara haipandi zilikuwa zimeichoka.

Hata hivyo Rais Samia hakukubali pendekezo la kupunguzwa kwa kiwango kinachokatwa katika mshahara wa mfaidika ili kulipia mkopo wa elimu ya juu, lakini akafuta riba ya asilimia sita iliyokuwa ikiongezwa kuendana na urudishwaji wa mikopo kwa kuchelewa. Ukiongeza kasi ya kurudisha ambayo tayari ilishaonekana, inaelekea kuwa hapo kuna suala la usimamizi, hivyo mwelekeo wa fikra ya CAG mstaafu kuwa mfumo wa mikopo ufumuliwe bado haikidhi mahitaji. Kwa nchi kama Tanzania ambako elimu ya juu ni gharama kubwa, si wazo baya kuhitaji waliofaidika kulipa zaidi kuwezesha elimu ya juu kwa wengine kwa njia ya mikopo, kwa msingi kuwa gharama za usimamizi wa suala hilo ziwe endelevu.

Endapo usimamizi na uongozi wa mikopo ni mbovu, wakuu wa vyuo au maofisa wa bodi wanafuja fedha za mikopo hewa, halafu bodi imejaa ajira zisizoeleweka, kama Utoah unaweza kusema kuwa mpangilio huo umeshindwa.

Suala hapa ni kuwa Utoah ana haki ya maoni yake lakini hakuna vyanzo vya kutosha kuyakinisha hoja kuwa ni kweli ufanisi wa mfumo wa bodi ya mikopo ni mdogo mno na hakuna haja ya kuendelea nao.

Ni wazi kuwa hisia hiyo bado ni changu ni ya wasomi zaidi na hasa wale wenye uwezo wa kupitia kwa kina nyaraka husika ikiwamo ripoti ya ukaguzi wa hesabu za serikali. Waliobaki ambao ni Watanzania wengi wameridhika.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Wanaowahudumia wenye ulemavu wanasema haya...

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS) inasema asilimia 10 ya Watanzania ni watu wenye ulemavu na pengine wanakadiriwa kufikia milioni tano na miongoni mwao wanawake ni asilimia 9.4 wakati wanaume ni asilimia tisa pia.

Aidha, NBS inasema asilimia 60 ya wanawake wenye ulemavu ndiyo wanaojua kusoma na kuandika na wanaume wakiwa ni asilimia 69 na hiyo inatokana na sababu mbalimbali ikiwamo wazazi kuwaficha watoto wenye ulemavu na ndani na kuwanyima haki nyingi ikiwamo elimu.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) mkoa wa Shinyanga, Richard Mpongo, mwenye uoni hafifu, anasema alipokuwa mtoto hakufichwa ndani wala wazazi wake hawakumwona kuwa ni mzigo, bali alipelekwa shule hadi akawa mwalimu na sasa ni mstaafu akieleza kuwa ana maisha mazuri.

"Pengine nisingepata elimu, maisha yangekuwa mabaya kwa vile wengi wenye ulemavu ambao hawakupata nafasi hiyo wengi maisha yao ni tegemezi na huomba msaada. Naomba wazazi iwe Shinyanga au popote tusiwafiche watoto ndani tuwapeleke shule ili wapate elimu na kuendesha maisha yao, wasiwadharau, mbona mimi nilipata elimu na ni naishi vizuri tu," anasema Mpongo.

"Sisi SHIVYAWATA Shinyanga tumekuwa tukipaza sauti kwa wazazi kupitia mikutano yetu mbalimbali kuwa wasiwafiche ndani watoto wanaoishi na ulemavu bali wawapeleke shule ili wakapate elimu na kumudu maisha yao kama wengine," anaongeza Mpongo.

Francisco Bega, Mwalimu Mkuu wa shule binafsi ya Brothers iliyopo Kitangili Manispaa ya Shinyanga, inayotoa elimu kwa watoto wenye ulemavu wakiwamo walio na mtindio wa ubongo, usonji na ulemavu wa viungo, anasema watoto hao wanastahili elimu kama walivyo watoto wengine.

Anasema shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 2019 baada ya kuona watoto wenye ulemavu wakinyimwa haki ya kielimu, wakizurura ovyo mitaani huku wengine wakifichwa majumbani ndipo wakaona ni vyema kuchukua jukumu la kuwasaidia kupata elimu.


Aidha, Bega anasema watoto hao wenye ulemavu kipindi wanapofika shuleni hapo kupata elimu wanakuwa hawajiwezi kwa lolote lile ikiwamo kujihudumia, huku wengine wakijisaidia na kuchafua nguo kutokana na kufichwa ndani muda mrefu na kusababisha akili zao kuzidi kudumaa.

"Nawaomba wazazi wenyewe watoto walio na ulemavu wabadilike wasiwaone watoto hao kama mkosi kwao watambue ni zawadi kutoka kwa Mungu, kama walivyo wengine wasifichwe ndani wala kuwatelekeza ovyo, wapelekeni kwenye shule maalum wakapate elimu kama wengine," anasema Bega.

"Mfano mzuri watoto hawa tulipowapokea walikuwa hawajiwezi kwa lolote lile wala kujihudumia wenyewe, lakini sasa hivi hawahitaji msaada wa mtu kila kitu wanafanya wenyewe na baadhi yao ambao walianza masomo zamani wanajua kusoma, kuhesabu na kuandika, " anaongeza Bega.

Mwalimu mlezi wa watoto wenye ulemavu shuleni hapo, Anna Geofrey, anasema watoto hao maendeleo yao ya kimasomo siyo mabaya, licha ya baadhi kukabiliwa na mtindio wa ubongo unaosababisha kupoteza kumbukumbu.

Mmoja wa wazazi Victoria Laurent, ambaye ana mtoto anayesoma katika shule hiyo maalumu ya Brothers, anasema kabla ya kumpeleka shule mtoto wake alikuwa hajimudu lakini sasa amebadilika kitabia na kimatendo.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi iliyoko katika Manispaa ya Shinyanga, Agnes Makambajeki, ambaye pia ana uoni hafifu, akiwafundisha wanafunzi wenye tatizo kama lake kwa kutumia machapisho ya nukta nundu. **PICHA: MARCO MADUHU**

> "Mfano mzuri watoto hawa tulipowapokea walikuwa hawajiwezi kwa lolote lile wala kujihudumia wenyewe, lakini sasa hivi hawahitaji msaada wa mtu kila kitu wanafanya wenyewe na baadhi yao ambao walianza masomo zamani wanajua kusoma, kuhesabu na kuandika, " anaongeza Bega.

Anasema wazazi wanapaswa kukubaliana na hali waliyonayo watoto wao wenye ulemavu, pamoja na kuwapeleka shule na siyo kuwaficha ndani bali wawatunze na kuwapatia mahitaji yao sawa na watoto wengine.

"Mtoto wangu alipokuwa ndani kabla sijampeleka shule alikuwa hawezi lolote lakini sasa hivi anajihudumia mwenyewe, anajua kusoma tofauti na hapo mwanzo, hivyo watoto hawa tuwapatie elimu ili watimize ndoto zao," anashauri Laurent. Agnes Makambajeki mwenye uoni hafifu ambaye ni Mwalimu Maalum katika Shule ya Msingi Buhangija Jumuishi katika Manispaa ya Shinyanga anasema alipelekwa shule na wazazi na hilo limemwezesha kuendesha maisha yake bila ya kumtegemea yeyote licha ya kuwa haoni.

Anasema watoto wenye ulemavu wana akili sawa na wengine, hivyo ni vyema wakapewa elimu sawa kupitia shule zinazohusika kama alivyosoma.

"Mimi licha ya kuwa sioni, taaluma yangu ni ualimu na nina fundisha watoto shuleni hapa wale wenye tatizo kama langu. Wako vizuri kweli kimasomo na matokeo ya mwaka jana ya darasa la saba wote walifaulu kwenda kidato cha kwanza, hivyo nawasihi wazazi wasiwanyime haki yao ya kielimu ili watimize ndoto zao kama mimi," anasema Makambajeki

Neema Mkanga ni Ofisa Elimu Manispaa ya Shinyanga, anasema haki ya kupata elimu ni ya kila mtoto na kuwataka wazazi wenye watoto walio na ulemavu, wawapeleke kwenye shule maalum, ikiwa walimu wapo wenye taaluma ya kuwafundisha na watafanya vizuri pamoja na kutimiza malengo yao.

Anasema kumficha ndani mtoto mwenye ulemavu siyo sahihi, bali wazazi wawapatie fursa ya kusoma ikiwa wameshuhudia watu wengi wenye ulemavu wana dhamana mbalimbali katika jamii, wengine wakiwa ni mawaziri na manaibu, hivyo wasiwabague wawapatie elimu.

SAYANSI
NA SABATO KASIKA

# Wadau sikieni, saidieni kuwafikia wabunifu, wavumbuzi wachanga

ILI kufanikisha juhudi za kukukuza ubunifu na uvumbuzi, mchango wa taasisi za sayansi na teknolojia, utafiti, vyuo vikuu pamoja na mamlaka mbalimbali zinazosimamia masuala ya kuwaendeleza na kuwaibua wabunifu na wavumbuzi ni eneo la kipaumbele.

Baadhi ya taasisi ambazo mchango wake na majukumu yake hayakwepeki ni pamoja na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (VETA), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) na Taasisi ya Ufundi na Maelezo ya Vijana ya Don Bosco.

Mchango wa wadau hao ni muhimu katika kusaidiana na serikali kufanikisha ukuaji wa kasi na wa kiufanisi wa sayansi ili jitihada zinazofanywa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia za kuwaibua na kuwatambua wabunifu wachanga zizae matunda ambayo pia ni endelevu, anasema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Waziri Mkuu anayasema hayo wakati akiziagiza taasisi kutumia ubunifu na uvumbuzi unaozalishwa nchini kama nyenzo muhimu wakati wa kuandaa na kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo inayoandaliwa na sekta zote.

Ni katika Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) yaliyofanyika wiki iliyopita, jijini Dodoma, Waziri Mkuu anapotoa wito huo na kuelezea umuhimu wa kukuza ubunifu na uvumbuzi kwa kushirikiana na wadau wote.

"Nitoe wito kwa taasisi zetu kutafuta , kusaidia na kutumia ubunifu na uvumbuzi unaozalishwa nchini kama nyenzo muhimu wakati wa kuandaa na kutekeleza mipango mbalimbali inayoandaliwa katika kila sekta iwe ya huduma au uzalishaji, ili kuongeza tija na kasi ya maendeleo ya nchi yetu," anasema Majaliwa.

Uvumbuzi, ubunifu na kazi za kisayansi zinaambatana na kuzifikisha kwenye uwanja wa kimataifa na huko ndiko kwenye suala la hatimiliki na Waziri Mkuu anaeleza kusikitishwa na idadi ya maombi madogo kutoka Tanzania ikilinganishwa na yale yanayotoka nchi jirani.

"Takwimu zilizotolewa na Shirika la Hatimiliki Duniani (World Intellectual Property Organization - WIPO) zinaonyesha, kwa mwaka 2020, Tanzania iliwasilisha maombi ya hatimiliki nane tu," kiwango ambacho ni tofauti ikilinganishwa na nchi moja ya jirani iliyowasilisha maombi ya hatimiliki 372, huku Afrika Kusini ikiwa imewasilisha maombi ya hatimiliki 1,514.

"Idadi hii ni ndogo sana, ninatarajia kuona mabadiliko katika eneo hili, haraka sana, ili wabunifu wote nchini waweze kupata hatimiliki za ubunifu wao ili kuendelea kuibua wabunifu na wavumbuzi zaidi," anasema.

Majaliwa anasema, kuna haja kuchukuliwa kwa hatua za makusudi za kuongeza hatimiliki za wabunifu na pia kuendelea kuibua na kuendeleza wabunifu na wavumbuzi wachanga kwa manufaa ya wahusika na taifa.



Waziri Mkuu akiangalia baadhi ya vifaa alipozindua mashindano ya ubunifu, jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

Waziri Mkuu pia anaiagiza Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kutimia nafasi yao kuwaelimisha wabunifu umuhimu wa kuhakikisha kuwa ubunifu na uvumbuzi wao unatambuliwa na kupewa hatimiliki.

"Elimu kuhusu hakimiliki ni muhimu, kwani itawawezesha wabunifu kulinda ubunifu wao. Wekeni mikakati ya kuwaelimisha wabunifu wachanga husasan walioko katika sekta isiyo rasmi kuwa na hakimiliki," anasema.



**KUIBUA WABUNIFU**

Wiziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, anasema, serikali itatenga bajeti ya kufanikisha Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu -MAKISATU ili kuibua wabunifu wapya kila kona ya nchi.

"Mashindano hayo hufanyika kila mwaka, yakidhaminiwa na wadau mbalimbali wa elimu, lakini serikali nayo kwa upande wake inajitahidi kuhakikisha inazidi kuyaboresha," Prof. Ndalichako anasema.

Anaeleza kuwa MAKISATU yanashirikisha wabunifu wa ngazi mbalimbali kuanzia vyuo vya ufundi, shule za msingi, vyuo vikuu na wabunifu binafsi kutoka kila kona ya nchi.

Waziri huyo anasema, kinachotakiwa zaidi ni wadau mbalimbali kushirikiana na serikali katika kuhamasisha harakati za sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuongeza mchango katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Anasema, ni muhimu kuendeleza mipango na mikakati ya kudumisha utaratibu wa kuwa na mashindano ya kitaifa ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili taifa liendelee kuwa na wabunifu na wavumbuzi wengi.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omar Kipanga, anasema wizara hiyo imekuwa ikiibua wabunifu na kukuza teknolojia miongoni mwa vijana, na kwamba hatua hiyo, inasaidia ukuaji wa uchumi wa nchi na kuongeza fursa kwa wabunifu kujipatia kipato.

Mwakilishi kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Godfrey Mulisa anasema, shirika hilo kwa kushirikiana na COSTECH limeandaa mradi uitwao Ufunguo, kwa lengo la kuendeleza ubunifu miongoni wa vijana.

Anasema maendeleo ya sayansi na teknolojia yanatajwa kuwa na fursa kubwa ya kuchagiza mchakato wa utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa (SDG's) iwapo yatatumiwa ipasavyo.

Anataja elimu mjumuisho yenye ubora na usawa kwa wote pia hukuza kujiamini, ujuzi katika ujasiriamali na uvumbuzi na kuendeleza uzalishaji wa fursa za ajira ambayo ni moja ya malengo ya umoja hasa lengo namba nane na kwamba Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHEMA) ina umuhimu wa kipekee kwa kuwa ndiyo nyenzo inayohitajika sasa kwa wabunifu na wavumbuzi nchini na Waziri Mkuu anataka itumike kuwaibua na kuwaendeleza wabunifu na wavumbuzi wachanga.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Utafiti wataja ulipo uwezeshaji endelevu kwa kaya maskini



Wanawake katika miradi ya biashara. **PICHA: MTANDAO**

MPANGO wa kuwezesha wanawake wa kaya maskini kiuzalishaji, utafutaji kipato, umiliki wa rasilimali na uongozi unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), unatajwa kuwa umefanikiwa, lakini inahitajika mikakati zaidi ili mafanikio hayo yawe endelevu.

Kuinua hali ya kinamama kupitia Mpango wa Kuwezesha Kaya Maskini (PSSN), kunaelezwa kuwa licha ya kufanikiwa kiuwezeshaji ni dhahiri kuwa, hakuna uhakika wa kuwa endelevu, pale mkakati huo utakapohitimishwa.

Ni kwa mujibu wa Dokezo la Utafiti wa Taasisi ya REPOA, toleo namba 2/2021 la Machi mwaka huu, na kwamba ili uwezeshaji uwe wa kudumu kunahitajika mikakati na mbinu mpya.

Mikakati hiyo mipya inahitajika ili kuingiza mafunzo ya stadi na ujasiriamali kwa walengwa na kuwaongezea uwezo wa kujipatia kipato na kujitegemea.

Aidha, utafiti wa REPOA unaongeza: "Uwezeshaji kupitia maendeleo ya wanawake, utafanikiwa zaidi ukiambatana na elimu ya uongozi na ushirikishwaji kwenye maamuzi ndani ya jamii."

Utafiti huo unapendekeza TASAF kufanya tathmini yakinifu ya maeneo ambako uwezeshaji umedhirika, kwa mfano kazi za ajira na nyinginezo zinazoambatana na ujira na kuyaongezea nguvu kifedha.

Aidha, unataka kupima ramani mpya ya umaskini nchini kubaini kaya zinazotishiwa kuingia kwenye dhiki au umaskini wa kupokezana kutoka kizazi hadi kizazi ili wahusika wasichwe nyuma. REPOA pia inaishauri TASAF kuongeza misaada kwenye maeneo yanayowaongezea wanawake uwezo wakujieleza na kushiriki kwenye maamuzi ndani ya jamii ili ongezeko la sauti yao liwasaidie kujiongezea uwezo kiuchumi na haki za kumiliki rasilimali.

Utafiti huo unapendekeza kutafuta njia za kupanua wigo ili kuwaingiza kwenye mfumo wajane, wanaume wenye majukumu ya kutunza kaya zisizojiweza na wale ambao wamekumbwa na umaskini wa kurithi.

Halikadhalika, inaitaka TASAF kuingiza kwa uwazi zaidi maswali ya usawa wa jinsia kwenye miradi ya PSSN na kushirikiana na asasi za kiraia kuwaelimisha walengwa kuhusu haki na usawa wakijinsia.

UWEZESHAJI WANAWAKE

Katika miradi mingi ya TASAF kwa vile kwenye kaya nyingi zilizolengwa huduma za kijamii hutolewa na wanawake, utafiti wa REPOA ulijielekeza kwenye kuchunguza ni kwa kiwango gani fedha na misaada ya TASAF kupitia PSSN ulivyochangia kwenye uwezeshaji wanawake kwa kuwaongezea uwezo kiuchumi, kisiasa na kuboresha mchango wao kwenye maendeleo yao binafsi, ya kaya na jamii.

Aidha, ulilenga kupima kiwango cha uwezeshaji wa wanawake wa kuwajengea uwezo wa kaya maskini na kuangalia kama fedha yenye masharti inayotolewa kwa walengwa hao ina mchango wa moja wa moja wa kuwawezesha wanawake.

Kadhalika dokezo la utafiti, lilisema ulitumia takwimu na taarifa kuhoji walengwa kwenye kaya 1,935 wakiwamo zaidi ya washiriki 11,000 wanawake kwa wanaume wenye zaidi ya miaka 18 katika wilaya tisa zilikoanzia shughuli za awali za TASAF zilizokuwa chini ya mpango wa TASAF's Program Authority Areas (PAA) kwa kipindi cha miezi 36 tangu kuanzia Novemba 2014 .

REPOA inasema vijiji 102 kwenye wilaya 11 vilifanyiwa utafiti zikiwamo kaya 15 hadi 18 kwa kila kijiji, ambazo zilichaguliwa kwa kutumia vigezo maalumu.

Wilaya zilizohusika kwa Tanzania Bara ni pamoja na Misungwi, Kahama, Kilosa, Kisarawe, Handeni, Mbogwe, Itilima,Uyui, Bagamoyo na Chamwino wakati visiwani Zanzibar wilaya moja ilihusika.

**MATOKEO YA UTAFITI**

Ushirikishwaji wanawake kwenye uzalishaji uchambuzi wa matokeo ya utafiti wa awali wa mwaka 2014 ulionyesha kuwa wanaume walikuwa na uwezo zaidi ya wanawake.

Hata hivyo, uchambuzi wa matokeo ya utafiti wa mwaka 2017 ulionyesha kwamba TASAF kupitia PSSN imewawezesha wanawake, aidha uchambuzi wa uwezeshaji huo kwenye maeneo tisa ulibaini kuwa uwezo wa wanawake ulikuwa bado chini ya ule wa wanaume kwenye maeneo saba ingawaje kwenye masuala yanayohusu matengenezo ya nyumba, jinsia zote mbili zilikaribiana sana na ushiriki wa wanawake kwenye shughuli za kaya ni mkubwa zaidi ya ule wa wanaume.

Utafiti wa REPOA unaonyesha pia kwamba kwa kulinganisha matokeo ya utafiti wa awali na ule uliofuata, vitu vitatu vilijitokeza, kwenye maeneo ya uvuvi, kilimo cha mazao ya biashara, ushiriki wa wanawake kwenye matokeo ya awali ulikuwa chini na kwenye matokeo ya utafiti wa pili uligundua kuwa uliendelea kushuka. Wakati kwenye kilimo cha mazao ya chakula takwimu za ushiriki hazikuwa na mabadiliko yoyote.

Kwenye ufugaji, kazi za kuajiriwa, shughuli zisizo za kilimo, akiba ya fedha na matengenezo ya nyumba, ushiriki wa wanawake umeongezeka kwa kiasi kikubwa na kuzidi ule wa wanaume. Kwa mfano, kwenye ufugaji awali matokeo yalionyesha kwamba ushiriki ulikuwa kwa asilimia 95.8 lakini matokeo ya utafiti wa sasa yakaonyesha kuwa ushiriki wao ni asilimia 100.99, kwenye kazi za kuajiriwa idadi ilipanda kutoka asilimia 95.8 hadi 165.70 na katika eneo la shughuli zisizo za kilimo kinamama walishiriki zaidi kutoka asilimia 98.6 za utafiti wa awali hadi kufikia asilimia 156.77.

Aidha, REPOA imebaini kuwa kwenye shughuli za TASAF za kujikimu kinamama walishiriki zaidi kwa ongezeko la kutoka asilimia 107 hadi 143 .74, wakati kwenye kuweka akiba ya fedha walifanya vizuri zaidi tena kwa kupanda kiwango kutoka asilimia 95.08 hadi asilimia 193.91 na kwenye kutengeneza makazi (nyumba) walikuwa juu kwa asilimia 158.26 ikilinganishwa na matokeo ya utafiti wa awali ambako walikuwa asilimia 100.

Ushiriki wa kinamama kwenye maamuzi na masuala yahusuyo matumizi ya fedha ni eneo ambalo lililoangaziwa na kwenye awamu zote za utafiti washiriki waliulizwa kiasi cha mchango wao kwenye maeneo tisa na kubainika kuwa wanaume walikuwa na mchango mkubwa zaidi. Eneo la mifugo na akiba ya fedha mchango wa wanawake na wanaume ulikuwa karibu sawa. Hata hivyo, kwenye shughuli za PSSN mchango wa kinamama ulikuwa mkubwa kuliko wa wanaume.

Kwenye maamuzi kuhusu matumizi ya kipato kinachotokana na PSSN utafiti ulibaini kuwa mchango wa wanawake ulikuwa zaidi ya wanaume, wakati masuala yanayohusu maamuzi kuhusu kipato takwimu zilizotokana na utafiti wa awali zinaonyesha kuwa wanaume walikuwa na mchango mkubwa kuliko kinamama hasa kwenye njia za kutengeneza mapato lakini kwenye mapato ya PSSN wanawake walikuwa na mchango mkubwa kwenye maamuzi ya matumizi.

Ili mafanikio hayo yawe endelevu REPOA inataka kubuniniwa mikakati zaidi ikiambatana na elimu kwa walengwa.



# Serikali kushirikiana na UDSM kutafiti kilimo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

SERIKALI imesema itashirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kufanya utafiti wa masuala ya kilimo, ili kukuza sekta hiyo inayotegemewa na watu wengi nchini.

Waziri wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, alibainisha hayo juzi katika warsha ya utafiti unaohusu kuchochea manufaa na ushirikishwaji wa wananchi katika fursa ya miradi mikubwa ya uwekezaji iliyoandaliwa na UDSM.

Alisema pamoja na kuwa wanafikia ukingoni katika mradi huo bado wizara yake itaendelea kuwatumia katika ufanyaji utafiti kwenye masuala ya kilimo.

Prof. Mkenda alisema serikali inatambua umuhimu wa utafiti unaofanywa na vyuo vikuu katika sekta ya kilimo, na warsha hiyo ina umuhimu mkubwa kwa kuwa itasaidia wakulima kuondokana na kero wanazokutana nazo katika kilimo.

Alisema wakulima wadogo ni muhimu kwa sababu wana mchango mkubwa katika kilimo na wao kujua nini wanatakiwa kufanya ili kuondokana na kero wanazokutana nazo katika kilimo.

"Kilimo ni suala muhimu sana kwa wananchi kwa sababu asilimia kubwa inategemea kilimo, hivyo nawapongeza UDSM kwa kuandaa warsha hiyo ambayo inawapa uelewa wakulima namna ya kuinuka kiuchumi," alisema Prof. Mkenda.

Naye Mhadhiri wa UDSM, Dk. Hezron Makundi, alisema mradi wa SAGOT ni wa miaka miwili, ulianza mwaka 2019 na unaishia Juni mwaka huu ukiwa na lengo la kutambua fursa za jamii kwa wawekezaji katika kilimo.

Dk. Makundi alisema mradi huo ambao unahusisha sekta binafsi wadau wa maendeleo pamoja na serikali, una maeneo makubwa matatu, ambayo ni kazi, ajira na uwajibikaji.

Alifafanua kuwa unapokuwa na mwekezaji ni lazima kumtazama kama mzuri au mnufaishaji kwa kutazama suala la ajira, ikiwa katika namna ya kila mwananchi ana nafasi ya kutaka uwekezaji katika masuala ya kilimo.

"Katika utafiti wetu tumeangalia hilo na tumeona kuna uwekezaji mwingine ni mzuri kwa sababu unaleta manufaa kwa wananchi, lakini mwingine sio mzuri kutokana na kutoinufaisha jamii," alisema Dk. Makundi.

Hata hivyo, alisema serikali inapaswa kuangalia namna ya kutengeneza mfumo ambao utakuwa unaangalia vitu hivyo muhimu ambavyo mwekezaji anapaswa kuvifanya ili kuinufaisha jamii katika uwekezaji wake.



Mbunge wa Jimbo la Mtama, Nape Nnauye, akichangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2021/2022 iliyowasilishwa jana, Bungeni jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waendesha bodaboda wapewa mafunzo

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

ZAIDI ya vijana 200 wanaojishughulisha na usafirishaji wa abiria kwa bodaboda na pikipiki za miguu mitatu, wamepewa mafunzo ya namna ya kujiongezea kipato yaliyotolewa na Benki ya NMB.

Lengo la mafunzo hayo ni kuwapa elimu ya mikopo inayotolewa na benki hiyo katika mpango wao wa miliki chombo na NMB ambao umetenga Shilingi bilioni tano katika kundi hilo.

Wengi wa vijana hao walikuwa wahitimu wa vyuo vikuu ambao waliamua kujiajiri kupitia bodaboda na pikipiki za miguu mitatu. Hata hivyo, wameiomba NMB kuangalia upya sharti la mtu kuwekeza asilimia 20 ndipo akopeshwe kwa kuwa vijana wengi wanakosa fursa hiyo.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa mikopo ya pikipiki za miguu miwili na mitatu, mwendesha bodaboda wa jijini hapa, Chacha Marwa, alisema mpango wa NMB ni mkombozi kwa vijana ambao wanaanza maisha kwa kuwa utasaidia kuwapatia vifaa vya kuwaingizia fedha.

Marwa ambaye ni mhitimu wa Shahada ya Sayansi ya Baiolojia ya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), alisema mpango wa kusubiri ajira unawachelewesha na kuwapotezea malengo vijana wengi, lakini kwenye bodaboda na pikipiki za miguu mitatu kuna fedha zaidi ya mshahara.

Akizungumzia asilimia 20 ambazo zinatakiwa na NMB kama dhamana ya mkopo, alisema kiasi hicho kinawakosesha sifa vijana wengi licha ya kuwa wana uwezo wa kurejesha, lakini ni pale wanapoanza maisha huwa hawana kianzio.

Kwa mujibu wa Chacha kama benki ingetengeneza utaratibu wa kuwapatia vijana bila kuweka hiyo asilimia, ingekuwa mkombozi mkubwa kwa vijana wengi ambao huzunguka na vyeti kusaka ajira bila mafanikio.

Meneja wa NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, alisema 'miliki chombo na NMB' imeshafika katika mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza na Dodoma na sehemu kubwa inalenga vijana wanaoanza maisha.

Alisema benki hiyo hutumia kero zinazojitokeza kwa Watanzania na kuwapelekea mawazo ya kuwa fursa na mambo mengi wanayozungumza vijana yanafanyiwa kazi kwa kufuata taratibu.

Kwa upande wake, Naibu Meya wa Jiji la Dodoma Emmanuel Chibago, aliomba benki kuwawezesha vijana hao kupitia Umoja wa Mabajaji na Pikipiki Dodoma (UMAPIDO) kwa kuwa wamekuwa wasimamizi wazuri kwa wanaokopa.

Chibago alitoa mfano wa mwaka jana Halmashauri ya Jiji la Dodoma ilitoa mkopo kwa UMAPIDO wa Sh. milioni 305, lakini hawajawahi kuchelewesha marejesho na kila mwezi wanarejesha Sh. milioni 12.5.

# 'Watoto wenye ulemavu wakoseshwa haki ya elimu'

**Na Peter Mkwavila,** BAHI

WATOTO wenye ulemavu wilayani Bahi, mkoani Dodoma bado wanakabiliwa na ukatili wa kijinsia wa kufichwa ndani na kukosa haki zao za msingi ikiwamo kwenda shule.

Diwani wa Kata ya Bahi, Augostino Ndovu, alibainisha hayo kwenye mkutano wa uhamasishaji kuhusu mradi wa elimu jumuishi uliofanyika katika kata hiyo.

Mpango huo wa elimu jumuishi unaratibiwa na Kanisa la Free Pentecostal Church Tanzania (FPCT) kwa kushirikiana na Information Center on Disability (ICD), ambao umewezesha watoto wenye ulemavu wa wilaya ya Bahi na Dodoma mjini kupata elimu ya msingi na awali.

Ndovu alisema bado kuna ukatili wanaofanyiwa watoto wenye ulemavu wa kufungiwa majumbani na kuwasababishia kuwanyima haki zao za msingi.

Kutokana na hali hiyo, diwani huyo aliwataka wananchi wa kata hiyo kutoa ushirikiano kwa wadau wa elimu jumuishi ambao wamekuwa mkombozi mkubwa kwenye familia za watoto wenye ulemavu.

Alisema bado kuna ukatili wanaofanyiwa watoto wenye ulemavu wa kunyimwa fursa ya kupata elimu ya awali na msingi.

"Kufikiwa na mradi huu wa elimu jumuishi utasaidia wazazi na walezi kufanya shughuli zao za kujipatia kipato wakati watoto wakiwa shule kufungiwa ndani tena kama ilivyokuwa awali," alisema.

Aliwashauri wazazi, walezi na wapenda maendeleo, kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa wadau wa elimu ambao wamekuwa wakiwaibua na kuwaokoa watoto wanaoishi mitaani na wanaofungiwa majumbani.

"Bado kuna changamoto kwa baadhi ya wazazi na walezi, kwa kuwa na mtizamo hasi, ambao wanaoendelea kuwafungia majumbani watoto wenye ulemavu kwa madai kuwa ni mkosi kwenye familia husika," alisema.

Sara Mazengo akizungumza kwa niaba ya wazazi wenye watoto wenye ulemavu, alisema kutokana na watoto wao kupelekwa shule na kupatiwa mahitaji maalum wao pia wameweza kujishughulisha na uzalishaji mali.

"Wazazi wengi tulikuwa tunahitaji kufanya shughuli zetu za uzalishaji mali kama vile za kilimo na ujasiriamali tulikuwa tukiwafungia watoto hao bila uangalizi wowote hali ambayo ilikuwa tukiwahatarisha usalama wao."

"Ila kwa sasa toka mradi huu wa elimu jumuishi ulipoanza kuwatambua watoto hao na kuwapeleka shule hivi sasa wazazi na walezi tulio wengi tunajishughulisha na kujipatia kipato," alisema.

Mratibu wa mradi huo, Jane Mgidange, alisema pamoja na kuwatambua watoto hao na hatimaye kuwapeleka shule pia wamekuwa wakihakikisha wanashirikiana na serikali kutatua kero wanazokabiliana nazo.



## Wajasiriamali waagizwa kusajili bidhaa zao

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAJASIRIAMALI mkoani Mbeya, wameagizwa kusajili bidhaa wanazozalisha katika mamlaka husika kwa lengo la kudhibiti ubora na kutambulika kwenye masoko ya ndani na nje ya nchi ili kuchangia mapato ya serikali.

Kauli hiyo ilitolewa juzi na Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Uchumi na Uzalishaji, Said Madito, wakati akizungumza na wajasiriamali pamoja na watumishi wa kampuni tanzu serikali ya Gs1 kuhusu umuhimu wa kusajili bidhaa wanazozalisha ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa masoko kulingana na ubora wa bidhaa.

Alisema serikali inataka kuongeza mapato kutokana na shughuli za kiuchumi na umefika wakati kila mjasiriamali na wafanyabiashara kusajili bidhaa zao ili kuchangia mapato na kutambulika katika masoko makubwa ndani na nje ya nchi.

Madito alisema bidhaa nyingi zinazozalishwa na wajasiriamali nchini hazijasajiliwa na kuisababishia serikali kukosa mapato na kuzitaka mamlaka husika za serikali zitoe elimu ili wajue umuhimu na kupanua wigo wa walipakodi ikiwa ni pamoja na kuingiza bidhaa katika masoko ha ushindani.

Mjasiriamali wa bidhaa za usindikaji, Selina David, kutoka Mkoa wa Njombe, alisema kabla ya kuhamasishwa na kupewa elimu ya kuongeza thamani ya mazao, alikuwa akiuza kwa mazoea.

Alisema sasa ameanza kuongeza thamani ya bidhaa anazosindika na atahakikisha anashirikiana na mamlaka husika ili kupanua wigo wa kupata mauzo makubwa na masoko ya uhakika.

"Miongoni mwa vikwazo vinavyotukabili ni elimu hivyo serikali iwekeze zaidi kuwafikia wajasiriamali wengi zaidi ili kuwawezesha kusajili bidhaa zao hususan mazao ya chakula na biashara yanayozalishwa nchini," alisema David.

Ofisa masoko wa Gs1, Dorcas Emmanuel, alisema taasisi hiyo ipo chini ya serikali na lengo la kutoa elimu ni kutokana na vikwazo vinavyowakabili wajasiriamali kuendesha biashara zao kwa mazoea na kukosa masoko rasmi kutokana na kutotambulika na kukosa ubora unaotambulika.

# Vibali 13 vyatolewa utekelezaji mradi umeme

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

MAMLAKA ya Bonde la Ziwa Nyasa, katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, imetoa vibali 13 vya kuanza utekelezaji wa mradi wa uzalishaji wa umeme megawati 50.34 kupitia maji ya Mto Rungwe ikiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali ili kuwa na uhakika wa nishati ya umeme.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Idara ya ufuatiliaji na tathmini Bonde la Ziwa Nyasa, Mhandisi John Kavishe, wakati Kamati za mabonde ya maji ilipotembelea mradi wa kituo cha taarifa ya hali ya maji katika Bonde la Mto Kiwira, unaomwaga maji katika Ziwa Nyasa.

Mhandisi Kavishe alisema mpaka sasa wametoa vibali 75 vya uwekezaji mbalimbali na kati ya hivyo, 13 vya uzalishaji nishati ya umeme megawati 50.34 na utekelezaji wake unaanza hivi karibuni baada ya kukamilika utahudumia wananchi wote wa Wilaya ya Rungwe.

"Uwekezaji wa vituo hivi vya taarifa za maji ni ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na mataifa mengine yaliyo Kusini ya Afrika (SADC) na kwamba vinawezesha wataalamu kujua viwango vya maji yakipungua na kuongezeka licha ya kuwapo kwa upungufu unaotokana na shughuli za kijamii," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Taifa, Dk. Halima Kiwango, alisema wametembelea chanzo cha maji cha Kiwira pamoja na daraja la Mungu na wamejionea namna maji yalivyorejea kwa wingi na kuleta uwezekano mkubwa kwa Wizara ya Maji kutekeleza miradi hususani ya umeme na kupata wawekezaji wakubwa katika miradi ya kilimo na ufugaji.

"Nimefurahishwa na usimamizi mzuri wa rasilimali hii ya maji katika Mto Rungwe, kimsingi miaka iliyopita kulikuwa na upotevu mkubwa wa maji, kikubwa wataalamu wa bonde mtunze kituo hiki cha taarifa ambacho tayari mmetoa vibali vya uzalishaji wa nishati ya umeme, kilimo pia ni vyema elimu iendelee kutolewa kwa wananchi lli kuachana na shughuli za kijamii katika mito na vyanzo vya maji.

Alisema kuwa vikwazo vikubwa walivyoviona katika mto Rungwe ni upotevu wa maji siku hadi siku na kushauri ni vyema iwekwe mipango madhubuti kuondokana na tatizo hilo kwa jamii ili wataalamu wa Bonde la Ziwa Nyasa waweze kufikia malengo ya kusogeza uwekezaji katika nishati ya umeme.



Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, akifungua kikao kazi cha Maofisa Habari, Mawasiliano na Uhusiano wa Serikali kinachofanyika kwa siku nne katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbarali yapunguza uhaba madawati kwa 80%

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbarali, imepunguza uhaba wa madawati katika shule zake za sekondari kwa zaidi ya asilimia 80 baada ya Mbunge wa jimbo hilo, Francis Mtega, kuamua kutumia fedha zote za mfuko wa jimbo kutengeneza madawati na kuyasambaza shuleni.

Mbunge huyo aliamua fedha zote zaidi ya Sh. milioni 70.9 zitumike kuchonga madawati na 875 yalipatikana.

Akizungumza wakati wa kukabidhi madawati hayo serikalini, Mtega alisema, aliamua kuelekeza fedha hizo kwenye sekta ya elimu akiamini kuwa sekta hiyo ina kero nyingi ambazo zinahitaji ufumbuzi wa haraka. "Natambua kuwa jimbo langu linazo kero nyingi, lakini nimeamua nianze na kero za kwenye sekta ya elimu ambazo athari zake zinawakumba wazazi na watoto pia, lakini najua kuwa elimu ndio msingi wa maendeleo, hivyo tukimaliza kero kwenye sekta ya elimu tutakuwa tumeweka mazingira mazuri ya kujiletea maendeleo," alisema.

Akipokea madawati hayo, Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema mahitaji ya madawati katika wilaya yote ya Mbarali ni makubwa na kwamba uamuzi alioufanya mbunge wa kuelekeza fedha za mfuko wa jimbo kwenye utengenezaji wa madawati ni mzuri wenye nia ya dhati ya kusaidia sekta ya elimu. Hata hivyo, aliwataka wananchi kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya elimu ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanaoandikishwa darasa la kwanza na wanaofaulu mtihani wa taifa wa darasa la saba wanapata vyumba vya madarasa wanapoanza masomo.

Alishauri uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kutoa maelekezo kwenye ngazi ya kata ya kuwataka watendaji kukusanya michango ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na miundombinu mingine wakati wa mavuno ili kila mwananchi aweze kuchangia bila shida.

"Kwa kawaida tumekuwa tukikimbizana kujenga vyumba vya madarasa kuanzia mwezi wa 12 na Januari baada ya matokeo ya mitihani ya taifa kutangazwa, lakini kipindi hiki pia huwa ni wakati wa kilimo, nashauri michango ya ujenzi na hata ujenzi wenyewe uwe unaanza mapema kuanzia mwezi Juni au Julai wakati ambao pia wakulima huwa wana uwezo mzuri wa kuchangia kwa sababu huwa wako kwenye mavuno," alisema Mfune.

Alisema wananchi wanapotakiwa kuchangia kuanzia mwezi Desemba au Januari huwa wako kwenye msimu wa kilimo na pengine baadhi yao huwa tayari wameshauza mazao muda mrefu na kutokuwa na fedha, jambo ambalo huathiri kasi ya ujenzi wa miundombinu ya elimu.

Katika makabidhiano hayo, Mbunge wa Mbarali, Mtega alitoa tuzo kwa walimu ambao wanafunzi wao walifanya vizuri kwenye mitihani ya taifa ya darasa la nne na darasa la saba katika shule za msingi na pia kwa walimu ambao watoto walifaulu vizuri mitihani ya kidato cha pili na cha nne katika shule za sekondari wilayani Mbarali.

Tuzo hizo ambazo ziliwafikia walimu wa shule za msingi na sekondari wapatao 67 kutoka wilaya nzima ya Mbarali zilikuwa na thamani ya zaidi ya Shilingi milioni tano, pia mbunge huyo aliahidi kuongeza dau kwa walimu watakaofanya vizuri mwakani.



# SMZ yatambua maeneo 43 hatarishi kwa mafuriko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema zaidi ya maeneo 43 yametambuliwa rasmi kuwa ni hatarishi na hayaruhusiwi wananchi kujenga nyumba za makazi kutokana na tishio la mafuriko.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Sakum Mohamed, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Uzini, Haji Shaaban Waziri, aliyetaka kujua maeneo yepi hatarishi ambayo wananchi hawaruhusiwi kujenga nyumba za kudumu.

Mohamed alisema kwa upande wa Unguja yapo maeneo 32 ambayo hayafai kwa ujenzi wa nyumba za kudumu ambayo yapo katika mabonde ya mashamba ya mpunga na maeneo yanayotuama maji.

Aliyataja maeneo hayo kuwa ni Mwera karibu na mabonde ya mpunga, Tomondo Ziwamaboga, Fuoni, pamoja na Bumbwisudi, Mkoa wa Magharibi Unguja.

Alisema licha ya wananchi kukatazwa kujenga nyumba katika maeneo ya bonde la mpunga la Bumbwisudi, wameonesha kukaidi agizo hilo na kutishia uhai wa maisha yao.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wananchi kwamba yapo zaidi ya maeneo 43 kwa upande wa Unguja na Pemba ambayo tumeyatangaza rasmi kwamba hayafai kwa ujenzi wa nyumba za kudumu za makazi ya wananchi kutokana na tishio la mafuriko ya maji katika kipindi cha mvua za masika," alisema.

Dk. Mohamed alisema serikali imeamua kuchukua hatua za tahadhari kuepuka mafuriko yanayoweza kujitokeza kama ilivyotokea miaka ya nyuma na maafa kusababisha hasara kubwa kwa wananchi.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhammed Said, akiwasilisha hotuba ya makadirio ya mapato ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 katika Baraza la Wawakilishi Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Serikali yakusudia kutoa mafunzo kwa wavuvi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uvuvi na Uchumi wa Bluu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imesema inakusudia kuanza kutoa elimu kwa makundi ya wavuvi na wananchi wanaoishi mwambao wa pwani kuhusu malengo na madhumuni ya mikakati ya serikali ya mapinduzi ya Zanzibar kuingia katika uchumi wa bluu.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu, Abdalla Hussein Kombo, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka, Issa Haji Ussi, aliyetaka kujua lini serikali itaanza kutoa elimu ya uchumi wa bluu kutokana na dhana hiyo kuwa mpya kwa wananchi.

Kombo alisema wanakusudia kuanza kutoa elimu kwa makundi mbalimbali kuanzia kwa wavuvi wa mwambao wa pwani kwa ajili ya kufahamu dhana ya uchumi wa bluu na vipi wananchi watanufaika kuvuna rasilimali ziliomo baharini kiuchumi.

Alisema wiki ijayo wanakusudia kuwakutanisha wadau katika kongamano litakalowakutanisha wavuvi wa Unguja na Pemba na kuelezea faida zitakazopatikana katika serikali kuingia uchumi wa bluu ambao umelenga kuwanufaisha wananchi kiuchumi.

"Mheshimiwa Spika nakubaliana na Mwakilishi ni kweli dhana ya uchumi wa bluu ni mpya, lakini wananchi ikiwamo wavuvi wengi hawaifahamu kikamilifu kwa hivyo wizara imejipanga kuwafikia walengwa kwa ajili ya kunufaika ikiwamo kuzingatia uvuvi haramu," alisema.

Alisema uchumi wa bluu utazingatia zaidi utunzaji wa mazingira ya baharini kwa ajili ya kunufaika na rasilimali ziliomo ikiwamo kupambana na uvuvi haramu.

"Mheshimiwa uchumi wa bluu malengo yake makubwa utakuwa ukizingatia utunzaji wa rasilimali za baharini kwa kutunza matumbawe ya baharini ambayo ndiyo mazalia ya samaki," alisema Kombo ambaye ni mtaalamu wa masuala ya usalama wa baharini na mikataba ya kimataifa.

# Vijana wasisitizwa matumizi bora ya TEHAMA

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIONGOZI wa Mwenge, Luteni Josephine Paul Mwambashi, amewata vijana kuitumia teknolojia ya TEHAMA kwa usahihi na uwajibikaji ili iwaletee faida badala ya matumizi mabaya ya kuyarejesha nyuma maendeleo ya taifa.

Akifunga kongamano la vijana mjini Unguja, alisema endapo watatumia teknolojia hiyo, itawaletea faida na kupata maendeleo chanya kwa taifa kutokana na kurahisisha upatikanaji wa elimu na malipo katika ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Alisema kumekuwa na wimbi kubwa la vijana wanaojishughulisha na utumiaji wa mtandao kinyume na taratibu kufanya utapeli wa fedha uchochezi udanganyifu, udhalilishaji wa kijinsia pamoja na kusababisha malezi mabaya kwa watoto na vijana.

Aliwataka vijana kuhakikisha wanatumia kwa usahihi TEHAMA ili kujenga taifa endelevu na kupata maendeleo kwa haraka.

Akizungumzia suala la mapambano dhidi ya maambukizi ya Ukimwi aliwataka vijana hao kuepuka vishawishi vinavyosababisha maambukizo ikiwamo kuachana na tamaa kwa kuwa ugonjwa upo katika jamii na unapunguza nguvu kazi ya taifa na kuwahimiza vijana hao kupima afya zao.

Alisema mbio za Mwenge zinasisitiza hasa mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana na bado ni tishio linaloathiri nguvu kazi.

Kadhalika, alisema mbio hizo zinasisitiza mapambano dhidi ya ugonjwa wa malaria ambao huwapata wajawazito na watoto na kutoa rai ya kufanya usafi wa mazingira yanayowazunguka ili kuua mazalia ya mbu pamoja na kutumia vyandarua vilivyowekwa dawa.

Akisoma risala, Ofisa Habari wa Wilaya ya Mjini, Msangu Said, alisema katika tasnia hiyo kuna changamoto ya upungufu wa ujuzi kwa vitendo ukosefu wa sera na taratibu ya kuondoa mali ya TEHAMA pamoja na kukosekana kwa wafanyakazi waliopata mafunzo.

Alisema kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amekusudia kuijenga Zanzibar mpya kupitia uchumi wa kisasa (Blue Economy) ambao una mpango mkakati wa kuendeleza wananchi na wafanyakazi kiujumla kuweka ufanisi na kuongeza thamani katika mfumo wa mazingira ya TEHAMA.

Kiongozi wa Mwenge alifungua miradi mbalimbali katika Wilaya ya Mjini ikiwamo mradi wa ufugaji samaki kwa vijana wa Shehia ya Bintihamrani, mradi wa maji Chumbuni na ufunguzi wa studio ya Stone Town.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**JESSY JACOB TEMU** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba S.1088/0116 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary TUMBI mwaka 2013, na cheti cha chuo cha **SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE** kozi ya **BACHELOR RURAL DEVELOPMENT** index namba **BRD/D/2016/0014** kilichotolewa mwaka 2019.yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/URA/RB/262277/2021**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ZAINABU YUSUFU TAHERALY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0843/0023** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **SOTELE** mwaka 2006, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi tarifa **UJMB/RB/312/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Mahakama ya Mwanzo ya.............. MJINI**

**Wilaya ya ...........................NYAMAGANA**

**Mdai.................................PENDO SIMBILA**

**Amdai**

**Mdaiwa ...ELIA ALPHONCE**

**Kwa......... k.k. MWENYEKITI MTAA WA MHANDU**

**Kwa kuwa mdaiwa/ wadaiwa ameleta madai yake/yao kwamba... MADAI YA TALAKA NA MGAWANYO WA MALI.**
**Kwa hiyo** unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii siku ya JUMA TANO Tarehe 26/05/2021 saa 2:30 Asubuhi kujibu madai haya na kwa kuwa siu hiyo ni siku ya kukatwa shauri unatakiwa kufika na mashahidi wako/ wenu na hati zote zinazo husu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria, hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shauri hii.itaweza kutoa hukumu umeshindwa/mmeshindwa. Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii tarehe 24/05/2021.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
MWANZA MJINI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO YA KAWE**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwazo KAWE**

**Usimamizi wa mirathi 134 2021**

**Ombi la BEATRICE ELITWAZA MAJEVU kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu MOSSES ISMAEL MALISA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 8/6/2021

Kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 8/6/2021

**Mahakama ya mwanzo**
**Kinondoni**
**Kimara**
**Sinza**
**Ilala**
**Temeke**
**Mbagala**
**Ukonga**
**Kigamboni**
**buguruni**

SAHIHI YA HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
KAWE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**(MAHAKAMA)**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ENABOISHU WILAYA YA ARUMERU**

**SHAURI LA JINAI/MADAI NA 14 YA 2021**

**VAILETH SAMFORD URASSA MDAI/MLALAMIKAJI**
**ELIREHEMA JACKSON SHAYO MDAIWA/MSHITAKIWA**
**HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMOS GENERAL)**
**(MCA Na. 2/1984)**

**Kwa ELIREHEMA JACKSON SHAYO-OLDADAI.**
**Kwa kuwa umelazimika uhudhurie mahakamani ili ujibu shitaka/madai kuwa shahidi kama ifuatavyo**

FIKA **MAHAKAMANI BILA KUKOSA KUJIBU MADAI YA TALAKA,MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO. UNAAMRIWA NA JAMHURI** uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya JUMATANO tarehe 2/6/2021 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa.
**USIKOSE KUHUDHURIA**
Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kuacha kuhudhuria mahakamani ni kosa **K/f Na. 114 A Sura 16 K/A**. Hivyo Mahakama inaweza kukuchukulia hatua kali za kisheria.
**HATI HII IMETOLEWA NA AMRI YANGU NA MHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 21/05/2021**

..........................................................
**HAKIMU.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.144/2021**

**Ombi la YUSTA LEINA MASAWE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu CANDIDUS NGALEKA NDUNGURU**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **27/05/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. **Tarehe 10/05/2021**

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MOROGORO

## KUPOKELEWA NA KADI YA GARI

**NDUGU SHAHID ROSHANALI FAZAL** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YAKE YA GARI AINA YA SUZUKI ESCUDO LENYE NAMBA ZA **USAJILI T103BBQ,** INJINI NAMBA **3S6504492** NA CHASSIS NAMBA **TD0IW141618.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOKO KARIBU NAYE, AU AWASILIANE NA MHUSIKA KWA **NAMBA 0769120142.** AMETOA TAARIFA POLISI NA KUPEWA NAMBA **KAG/BUK/RB/198080/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**AUGUSTINO ROBERT MMARI**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba ya usajili **T841AEQ**
**CHASSIS NO VRGE24654543**
**ENGINE NO TD27340104**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo Cha Polisi
Taarifa ya Polisi
**ARU/ARU/RB/233889/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GEORGE MICHAEL WAKUGANDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA ALPHARD** yenye namba za usajili **T 998 DVY** chasis namba **ANH 10-0162054,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa
**DAR/MAG/RB/233328/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SHABANI SAID NDESEME** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA SPACIO** yenye namba za usajili **T 764 CAB** chasisi namba **NZE 1213171993** engine namba **INZA657788,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa
**DAR/MAG/RB/8604/2020**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi NO.138/2021**

**Ombi la KAFALE SELEMANI MAHARAGANDE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu HATUJUANI ABDALAH MAHARAGANDE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 08/06/2021 kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 06/05/2021

Tarehe 6/5/2021
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MOROGORO

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# 15 wafariki kwa volcano, njaa ikitikisa

**Goma,** DRC

INAKADIRIWA watu 15 wamefariki kutokana na mlipuko wa volkano uliotokea katika Mlima wa Nyiragongo, mwishoni mwa wiki, Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Inaelezwa huenda vifo vikaongezeka wakati maofisa wakiyafikia maeneo yaliyoathirika zaidi.

Katika tangazo lililotolewa jana, serikali ya kijeshi ya mkoa wa Kivu ya Kaskazini, ilipiga marufuku shughuli zote za shule na kuwataka wazazi kuwalinda majumbani watoto wao.

Mamlaka zilisema idadi kubwa ya watoto wametengana na familia zao na wengine kukanyagwa.

Ukosefu wa chakula umejiri baada ya maghala na masoko ya vyakula katika maeneo kadhaa Goma, kushuhudia upungufu mkubwa wa vyakula tangu jana Jumapili siku moja tu baada ya mlipuko.

Volkano ililipuka katika mlima Nyiragongo na kumwaga uji wa moto ama lava, anga kuwa jekundu ingawa lava haikufika katika mji huo, ulio na watu milioni mbili, Kusini mwa mlima huo.

Wakazi wa vijiji vya karibu na mlima walioyakimbia makazi yao wameanza kurejea huku wengi wao wakiwasaka jamaa zao waliopotea.

Watu tisa miongoni mwa waliothibitishwa kufa, walipoteza maisha katika ajali za barabarani wakati watu walipokuwa wakihaha kukimbia ili kuokoa maisha yao.

Wanne walikufa walipokuwa wakijaribu kutoroka gerezani na wawili wakiungua hadi kufa, alisema Msemaji wa Serikali, Patrick Muyaya.

Zaidi ya watoto 170 wanahofiwa kupotea na wengine 150 wametengana na familia zao, Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), lilisema litaweka vituo vya kuwapokea watoto watakaopatikana wakiwa peke yao.

Lava iliishia karibu na wilaya ya Buhene, viungani mwa mji wa Goma na kuangamiza mamia ya nyumba na hata majengo makubwa. Ukarabati unatarajiwa kuchukua miezi kadhaa.

"Nyumba zote zilizopo katika wilaya ya Buhene zimeungua," Innocent Bahala Shamavu aliiambia shirika la habari la kimataifa la Associated Press.

Kwingineko, lava ilikatiza katika moja ya barabara kuu inayounganisha Goma na mji wa Beni, ambayo ni njia muhimu ya usambazaji wa misaada.

Hata hivyo, uwanja wa ndege wa mji wa Goma haukuguswa na lava, kinyume na ripoti za awali kwamba uliathiriwa.

Mlima huo wa volkano uliopo kilomita 10 kutoka Goma, ulilipuka mara ya mwisho mwaka 2002 na kusababisha vifo vya watu 250, huku watu wengine 120,000 wakiachwa bila makazi.

Mlipuko wa volkano uliosababisha vifo zaidi ulitokea mwaka 1977, ambapo watu 600 waliuawa. **BBC**



Picha iliyopigwa kutoka angani, ikionyesha tope lililotokana na volcano iliyotokea kwenye Mlima Nyiragongo, mwishoni mwa wiki, mjini Goma nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Inakadiriwa zaidi ya watu 15 wamepoteza maisha. **PICHA: AFP**

## Upepo mkali sababu ajali Mkuu wa Jeshi Nigeria

**Lagos,** NIGERIA

RIPOTI za awali zimebaini kuwa upepo mkali, ulisababisha ajali ya ndege, aliyokuwamo Mkuu wa Jeshi la Nigeria Ibrahim Attahiru (pichani), ilipokuwa inatua.

Uchunguzi zaidi unaendelea kuhusu ajali hiyo.

Mkuu wa Jeshi la Nigeria, Ibrahim Attahiru, alikuwa safarini kuhudhuria sherehe ya mahafali ya maofisa wapya wa Jeshi wa Chuo cha Ulinzi mjini Kaduna, Kaskazini mwa Nigeria.

Ofisa wa Idara ya Anga Uwanja Ndege wa Kaduna, Amina Salami, alisema ndege hiyo ambayo ilikuwa imembeba Lt. Gen. Ibrahim Attahiru na maofisa wengine 10, ilipangwa kutua katika kituo cha jeshi ingawa, hali ya hewa ilisababisha ndege kwenda kutua katika uwanja wa kiraia ilikopata ajali hiyo.



Katika mazishi ya maofisa hao 11 mjini Abuja, Mkuu wa Majeshi wa Ulinzi, Jenerali Lucky Irhabor, alisema maofisa wote walipoteza maisha yao katika huduma kwa taifa, watabakia alama.

Waziri wa Ulinzi, Ibrahim Magagshi katika ujumbe wa Rais Mohammadu Buhari, alisema Nigeria, imepoteza maofisa wa jeshi ambao walikuwa wakishughulikia suala la umoja.

Luteni Jenerali Attahiru, alionyesha bidii yake katika kazi kutekeleza wajibu katika kufanikisha kazi zake, ikiwa ni juhudi za kulipunguzia nguvu kundi la Boko Haram. **VOA**

## Watu 14 wafariki ajalini Italia

**Piedmont,** ITALY

RAIA wa kigeni ni miongoni mwa waliokufa, kwenye ajali ya gari maarufu ya kubeba watalii.

Mamlaka haijatoa maelezo zaidi. Picha kutoka eneo la tukio zinaonyesha gari hilo likiwa kwenye mteremko unaoelekea kwenye ziwa.

Watu 14 waliuawa juzi mita 20 kwenda chini ya ziwa. Miongoni mwa watalii hao, alikuwamo mtoto ambaye alifariki akiwa hospitali baada ya kupata shinikizo la moyo.

Mtoto wa pili alijeruhiwa vibaya, ingawa alikuwa na fahamu na uwezo wa kuongea, kulingana na taarifa za hospitali.

Gari hilo ni ambalo linatumia waya liitwalo 'Stresa-Mottarone' linasafiri kati ya mji wa Ziwa Maggiore hadi juu ya mlima Mottarone wa mkoa wa Piedmont nchini Italia kwa takribani dakika 20.

Picha kutoka eneo la tukio zilionyesha gari hilo likiwa limejifunga kwenye mteremko unaoelekea kwenye ziwa.

Meya wa Stresa, Marcella Severino, aliliita eneo hilo ni la kutisha na alisema ajali hiyo inaweza kuwa imesababishwa na waya kukatika. **VOA**

## Marekani yawekea vikwazo Ethiopia mzozo wa Tigray

**Washington,** MAREKANI

MAREKANI imeweka vikwazo kadhaa vya kiuchumi na usaidizi wa kiusalama dhidi ya Ethiopia kufuatia mzozo wa eneo la Tigray.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, pia alitangaza marufuku ya usafiri dhidi ya maofisa wa Ethiopia na Eritrea, pamoja na wengine ambao wanatuhumiwa kufanya ukatili.

Blinken alisisitiza kuwa hatua ya kimataifa inahitajika ili kusaidia katika utatuzi wa mzozo huo na wale waliopewa dhamana ambao hawajachukua hatua madhubuti kukomesha ghasia.

Maelfu ya watu waliuawa na wengine kadhaa kuachwa bila makazi, tangu mzozo ulipozuka miezi sita iliyopita.

Gazeti la Telegraph la Uingereza limeripoti kuwa watu kadhaa walichomwa vibaya kutokana na matumizi ya phosphorous nyeupe. **BBC**



# GATTUSO ATIMULIWA NAPOLI

**NAPLES,** Italia

NAPOLI wameachana na Kocha wao Mkuu, Gennaro Gattuso, Jumapili baada ya kukosa nafasi ya kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Muda mfupi baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Hellas Verona pale kwenye dimba la Diego Armando Maradona, matokeo ambayo yameifanya Napoli kumaliza nafasi ya tano kwenye msimamo wa Serie A, Rais Aurelio De Laurentiis, alithibitisha kuondoka kwa Gattuso.

Napoli walikwenda kwenye mchezo huo wa mwisho wa ligi wakiwa nafasi ya nne, lakini baada ya Juventus kushinda 4-1 dhidi ya Bologna kukawaondoa kwenye nafasi hiyo.

Gattuso, ambaye mkataba wake ulikuwa unamalizika mwishoni mwa mwezi ujao, amekuwa akihusishwa na Fiorentina.

"Ndugu Rino, nina furaha kutumia kama misimu miwili na wewe," aliandika De Laurentiis kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Shukrani kwa kazi yako, nakutakia mafanikio mazuri popote uendapo. Msalimie mke wako na watoto wako."

Gattuso alichukua mikoba ya kuinoa timu hiyo Desemba mwaka 2019 baada ya kuondoka kwa Carlo Ancelotti.

# Guardiola: Aguero atajiunga na Barca

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amethibitisha kwamba, mshambuliaji Sergio Aguero atajiunga na Barcelona kipindi hiki cha majira ya joto.

Imeripotiwa kwamba, Aguero amekubali mkataba wa miaka miwili na miamba hao wa LaLiga hapo Barca akiwa mchezaji huru, mkataba wake na City unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Guardiola amethibitisha siri hiyo baada ya Man City kufunga mabao 5-0 dhidi ya Everton ambapo Aguero alicheka na nyavu mara mbili wakati wakikabidhiwa Kombe la Ligi Kuu England juzi, Jumapili.

"Nina uhakika kabisa, pengine ndio natoa siri, labda anakaribia kusaini mkataba na klabu ya moyo wangu, Barcelona," alisema Guardiola akiiambia BBC.

"Anakwenda kucheza pamoja na mchezaji bora wa muda wote, Lionel Messi. Nina uhakika anafurahia zaidi kucheza pale Barcelona.

"Nina uhakika atakuwa imara zaidi uwanjani na ataisaidia klabu kuwa imara na imara zaidi."

Aguero amekuwa na City tangu mwaka 2011, akicheza mechi 389 na kufunga mabao 260 ambapo amewekа rekodi klabuni hapo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ameshinda mataji 15 na City, yakiwamo matano ya Ligi Kuu England.

Aguero alishinda taji la Ligi Kuu na Kiatu cha Dhahabu msimu wa 2014-15 na alishinda mara mbili mchezaji bora wa City wa mwaka msimu wa 2011-12 na 2014-15.






# *Milan imestahili nafasi ya pili – Pioli*

**MILAN,** Italia

KOCHA wa AC Milan, Stefano Pioli, amesema kikosi chake kimestahili kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, baada ya kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, nafasi waliyoisubiri kwa muda mrefu, baada ya Jumapili kushinda mabao 2-0 dhidi ya Atalanta.

Pioli aliiongoza Milan kileleni mwa msimamo wa Serie A kipindi cha kwanza cha msimu wa 2020-21, lakini baadaye wakajikuta wakitupwa hadi nafasi ya tano, kabla ya kurudi ya pili.

"Tumefanikiwa kwa sababu tulistahili na tulistahili nafasi ya pili kwenye msimamo," alisema Pioli akiiambia Sky Sport Italia.

"Ilikuwa sawa, bahati mbaya tulipoteza pointi katika mechi tulizotakiwa kushinda, lakini mchezo wa mwisho tulipambana na kupata pointi zote.

"Kwa uhakika nina furaha kubwa na hilo, ni nafasi tuliyoipambania sana na hatimaye tumeipata."

Milan kumaliza nafasi ya pili kwenye msimamo huo, ni matokeo bora zaidi tangu msimu wa 2012-13 walipomaliza nafasi ya tatu."

# Pirlo: Nitaendelea kuwa kocha Juventus

**TURIN,** Italia

ANDREA Pirlo anatarajia kubakia Juventus kama kocha mkuu msimu ujao baada ya kuiwezesha kumaliza kwenye 4 bora.

Juve iliifunga Bologna mabao 4-1 Jumapili, ushindi ambao umethibitisha kwamba wamemaliza nafasi ya nne kwenye Serie A, pointi moja zaidi ya Napoli baada ya kutoka sare ya 1-1 na Hellas Verona nyumbani.

Ushindi kwa Napoli ungewafanya Juve kuwa nje ya nne bora bila kujadili matokeo ya 'Bianconeri' hao.

Ulikuwa ni mchezo wa mwisho wa Juve kama bingwa mtetezi na Pirlo alishindwa kuiongoza kushinda taji la 10 mfululizo.

Msimu uliopita Juventus walishinda taji la tisa mfululizo kwenye ligi hiyo ya Italia.

"Mara zote nimesema kwamba, nimejitoa kwa ajili ya kazi hii, na matokeo ya mwisho yameonyesha hivyo. Wale wote wanaoamua kuhusu majaliwa yangu, watafanya hivyo," alisema akiiambia DAZN.

"Najiona mwenyewe kama kocha wa Juve msimu ujao. Ninaweza kuthibitisha hilo mimi mwenyewe.

"Lakini sasa tunatakiwa tu kufurahia kile tulichoweza kukipata kwa msimu huu, kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya."



# MBAPPE AINYOOSHEA KIDOLE BODI PSG




**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe anataka bodi ya Paris Saint-Germain kufanya maamuzi katika soko la usajili baada ya Lille kuipiku na kutwaa taji la Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Mbappe alifunga bao lake la 27 kwenye ligi hiyo wakati wakishinda 2-0 dhidi ya Brest Jumapili kwenye mechi ya mwisho, lakini Lille wakawafumua Angers 2-1 na kubeba taji hilo.

PSG ilinyanyua Kombe la Coupe de France wiki iliyopita, lakini malengo yao kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya yalimalizwa na Manchester City kwa kutolewa hatua ya nusu fainali mwezi uliopita.

Mbappe mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu ujao na ameiambia Canal Plus angependa kuona mabadiliko katika kikosi hicho cha kocha, Mauricio Pochettino.

"Siwezi kusema nini kinachohitaji kufanyika, mimi ni mchezaji tu, lakini nafikiri watu wameona, kila mmoja ameona," alisema.

"Wakati kila mmoja anaona, ni rahisi kujua hatima, lakini hakuna tatizo. Tumepoteza taji, lakini sasa tunatakiwa kujikita kwa yajayo."

# Laporta, Koeman kuteta Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman atakaa chini kuzungumza na Rais wa Barcelona, Joan Laporta, wiki hii kuhusu majaliwa yake hapo Catalunya, kwa mujibu wa Diario Sport.

Msimu wa kwanza wa Koeman hapo Barcelona haukuwa wa kuvutia sana, hivyo kuibua mjadala kuhusu majaliwa yake.

Koeman aliisaidia Barcelona kumaliza msimu wa LaLiga wa 2020-21 wakiwa nafasi ya tatu, pamoja na kunyanyua taji la Kombe la Mfalme (Copa del Rey), lakini walitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16-bora.

Ulikuwa msimu wa mabadiliko hapo Barcelona, huku Laporta akichukua nafasi ya urais Machi mwaka huu na hivi karibuni alisema watafanya "marekebisho" makubwa mwishoni mwa msimu huu.


Koeman aliteuliwa na Rais aliyepita, Josep Maria Bartomeu, kwa mkataba wa miaka miwili Agosti mwaka jana.

Laporta pia anafikiria kuuza wachezaji zaidi ya 10 kipindi hiki cha majira ya joto ili kupata nyota wapya.

Barcelona imekuwa ikihusishwa na usajili wa wachezaji kadhaa akiwamo Sergio Aguero, Erling Haaland na Georginio Wijnaldum.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER: MAGUIRE SASA KUIKOSA FAINALI EUROPA

## Nitasubiri hadi Jumatano, anatakiwa kufanya mazoezi Jumanne, lakini kwa uhakika...

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesisitiza kuwa hatarajii nahodha wa Manchester United, Harry Maguire, kuwa fiti kwenye fainali ya Ligi ya Europa Jumatano hii.

Maguire aliumia kifundo cha mguu wakati wakishinda mabao 3-1 dhidi ya Aston Villa Mei 9, mwaka huu na alikosa michezo minne ya Ligi Kuu England msimu huu.

Nyota huyo wa kimataifa wa England amekuwa akitumia magongo na ilionekana kwamba anaweza kuwa kwenye mchezo wa fainali ya Europa dhidi ya Villarreal pale Gdansk, Poland.

**Hata hivyo, Solskjaer amekubali kwamba, kuna uwezekano mdogo wa kumtumia Maguire kwenye mchezo huo.**

"Nitasubiri hadi Jumatano," alisema kocha wa United baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Wolves Jumapili.

"Labda kama anaweza kufanya mazoezi Jumanne, lakini bado nafasi ni ndogo sana. Simtarajii yeye kuwa tayari kwa ajili ya mchezo huu. "Bila shaka, anataka kucheza lakini hilo litakuwa ni suala la daktari. Simtarajii yeye kuwa tayari.

"Haionekani lakini kwa uhakika ni pigo kubwa kwetu, lakini nina matumaini makubwa sana.

"Anatakiwa kufanya mazoezi Jumanne, lakini kwa uhakika kabisa hatuna uhakika kabisa."

## ZISIKUPITE

### TUCHEL AMTAKA KANE

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, anamtaka mshambuliaji wa Tottenham na England, Harry Kane, 27. ***(Telegraph)***

### MADRID, ZIDANE KUKETI

KOCHA wa Real Madrid, Zinedine Zidane atafanya mazungumzo na Real Madrid katika siku zijazo kuhusu mustakabali wake katika klabu hiyo. ***(ESPN)***

### SPURS KUMSAJILI WATKINS

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Chelsea, Tony Cascarino, ameidokezea Tottenham Hotspur kumsajili mshambuliaji wa Aston Villa, 25, Ollie Watkins ili awe pacha wake endapo Harry Kane ataondoka Spurs. ***(Talksport)***

### MARCELO MKATABA MPYA

LEEDS United wamekubali kuingia mkataba mpya wa mwaka mmoja na kocha wao raia wa Argentina, Marcelo Bielsa, 65, huku tangazo rasmi likitarajiwa kutolewa wiki hii. ***(Mirror)***

### RONALDO ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inamfuatilia kwa karibu mshambuliaji wake wa zamani, Cristiano Ronaldo aliyepo Juventus, huku "mawakala wanaofahamiana" na mshambuliaji huyo wa Ureno mwenye umri wa miaka 36, wakisema "anaweza kutaka kuondoka" katika klabu hiyo ya Turin. ***(Athletic)***

### LIVER KUMSAJILI BISSOUMA

LIVERPOOL wapo kwenye nafasi nzuri ya kumsajili kiungo wa Mali, Yves Bissouma, 24, kutoka Brighton. ***(Mail)***

### LIVERPOOL KUMKOSA KONATE

UWEZEKANO wa Liverpool kumsajili mlinzi wa RB Leipzig, Ibrahima Konate, 21, ni mgumu kutokana na kipengele cha kumuachia cha thamani ya pauni milioni 34 ambacho wanataka kilipwe chote. ***(Times)***

### WAJITOSA KWA WIJNALDUM

KLABU ya Paris St-Germain ni miongoni mwa timu zinazopigiwa upatu kumsajili kiungo wa kati wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum, 30, ambaye anaondoka Liverpool kama mchezaji huru. Barcelona bado hawajaweka wazi dau la kumuuza mchezaji huyo. ***(Le10Sport)***

### WAKOMAA NA ODEGAARD

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema Arsenal itaanza mazungumzo na Real Madrid kuhusu mkataba mpya kwa ajili ya kiungo wa kati anayecheza kwa mkopo hapo, Martin Odegaard, 22, "katika wiki chache zijazo ". ***(Sun)***

### MATA HAJUI HATIMA YAKE

KIUNGO wa Manchester United, Juan Mata, 32, hana uhakika kama ataendelea kusalia katika klabu hiyo baada ya mkataba wake kumalizika kipindi hiki cha majira ya joto. ***(Mail)***

## Mr. UK Marathon kusomesha wajasiriamali

**Na Sabato Kasika**

SEHEMU ya mapato ya mbio za Mr. UK Marathon 2021, inatarajiwa kutumika kuwasomesha wajasiriamali wadogo katika Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo nchini (SIDO) ili kuwaendeleza zaidi.

Mbio hizo za kilometa tano, 10 na 21, zinatarajiwa kufanyika Julai mwaka huu kwenye viwanja wa Leaders Club jijini Dar es Salaam zikishirikisha wakimbiaji wa ndani na nje ya nchi zikiwa na lengo la kuhamasisha uwekezaji.

Mratibu wa mbio hizo ambazo zinafanyika kwa mara ya kwanza nchini, Nelson Mrashan, alisema jijini Dar es Salaam juzi kuwa, zitahamasisha uwekezaji, na kwamba ni fursa kwa wajasiriamali wadogo kufaidika kwa kupatiwa mafunzo ya muda.

## Kaseba kuibua vipaji Kick Boxing

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa mchezo wa ngumi na mateke (Kick Boxing), Japhet Kaseba, muda si mrefu anatarajia kufanya mashindano ya kuinua vipaji vya vijana jijini Dar es Salaam, ameeleza.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, bondia huyo alisema kwa sasa vijana wote wanaendelea na mazoezi katika Gym ya Mwananyamala kwa ajili ya kuiweka sawa miili yao huku wakiendelea kusubiri kupangiwa tarehe na muda wa mashindano hayo.

"Hivi karibuni tunatarajia kuwa na mashindano ya vijana yatakayofanyika wilaya zote za Dar es Salaam, lengo likiwa ni kuinua vipaji vya vijana ambao wana uwezo lakini wanashindwa kuonekana kutokana na kukosekana uwezeshwaji," alisema Kaseba.

# SIMBA YAPANIA KUISHUSHIA HASIRA DODOMA JIJI FA CUP

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutolewa kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mabingwa wa Tanzania, Simba, jana wameingia rasmi kambini, kujiandaa na mechi ya robo fainali ya Kombe la Azam Federation (ASFC), maarufu Kombe la FA, dhidi ya Dodoma Jiji FC.

**Simba ambao ni mabingwa watetezi wa Kombe la ASFC, watashuka dimbani kesho, Jumatano kuwakaribisha wageni wao Dodoma Jiji FC, katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam majira ya saa 1:00 usiku.**

Mabingwa watetezi hao, watashuka katika uwanja huo wakiwa na kumbukumbu ya kufanya vizuri kwenye mechi iliyopita ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kaizer ya Chiefs ya Afrika Kusini, lakini wakatolewa kwa jumla ya mabao 4-3 kutokana na mchezo wa awali ugenini kupigwa 4-0.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, alisema wamerejea katika michezo ya nyumbani ambapo wataanza kucheza Kombe la ASFC, hivyo anaamini kadri michuano hiyo inavyozidi kusonga mbele ndio inakuwa migumu, jambo ambalo wanapaswa kujipanga vizuri.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanatetea ubingwa wa michuano hiyo kwa sababu wana kikosi bora na wanapaswa kudhihirisha hilo kwa kuhakikisha wanafanya vizuri dhidi ya Dodoma Jiji ili kusonga mbele na hatimaye kutetea taji lao.

"Haitakuwa mechi rahisi kwetu dhidi ya Dodoma Jiji, tuliweza kuwafunga kwenye mechi mbili za ligi, lakini haimaanishi hii itakuwa nyepesi, kwenye mashindano kadri yanavyozidi kupiga hatua yanakuwa magumu.

"Kikubwa ni maandalizi tunayofanya na kudhihirisha ubora wa kikosi chetu ni kuhakikisha tunapambana kila mechi kufikia malengo yetu kwanza kwa kucheza kwa nidhamu ya hali ya juu katika mchezo huo," alisema Gomes.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Clatous Chama, alisema baada ya kutolewa Ligi ya Mabingwa Afrika hawatapumzika bali wataendeleza makali yao kuhakikisha wanafanya vizuri na kutetea ubingwa wao ili msimu ujao kuiwakilisha tena nchi.

Alisema wameahidi kucheza kwa nguvu zote ili msimu ujao kuendelea kupambana na kuvuka katika hatua waliyoishia msimu huu ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Ligi ya Mabingwa imemalizika (kwa upande wetu), najivunia timu yetu kwa sababu kila mmoja wetu alijitoa na kufanya kazi nzuri, baada ya hapo hatutapumzika hadi tuhakikishe tunatimiza kile tunachokihitaji," alisema Chama.

Alisema watarejea katika michuano ya nyumbani kwa kasi ile ile ambayo walikuwa wakicheza kwenye michuano ya kimataifa kwa kuhakikisha wanashinda mechi zote zilizopo mbele yao wakianza dhidi ya Dodoma Jiji kesho.

Katika hatua ya nusu fainali, mshindi kati ya Simba na Dodoma Jiji, atacheza na timu itakayoshinda katika robo fainali nyingine kati ya Rhino Rangers na Azam FC.




Bondia wa Nigeria, Alanrewaju Durodoro (wa pili kushoto) na kocha wake, Adefemi Babafemi (wa pili kulia), wakiwasili Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere tayari kwa pambano la Ijumaa dhidi ya Shaaban Jongo wa Tanzania katika Rumble in Dar 2 litakalofanyika Ukumbi wa Next Door Arena jijini Dar es Salaam. Wengine katika picha ni maofisa wa Kampuni ya Jackson Group Sports waandaaji wa pambano hilo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Bondia Jongo atamba kutwaa ubingwa wa ABU

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

BONDIA wa uzito wa juu wa ngumi za kulipwa nchini, Shaaban Jongo, ametamba kumsambaratisha mpinzani wake kutoka Nigeria, Alanrewaju Durodoro, katika pambano la kuwania Ubingwa wa Afrika (ABU) lililopangwa kufanyika Ijumaa wiki hii kwenye Ukumbi wa Next Door Arena jijini Dar es Salaam.

Mabondia hao watapigana katika pambano la utangulizi la raundi 10, ambapo siku hiyo bondia Hassan Mwakinyo atazichapa na Muangola Antonio Maiala, kuwania Ubingwa wa Afrika wa (ABU) wa uzito wa super welter katika pambano hilo lililoandaliwa na Kampuni ya The Jackson Group Sports chini ya Ofisa Mtendaji Mkuu, Kelvin Twissa.

Jongo alisema amejiandaa vizuri na pambano hilo na kamwe hatamdharau mpinzani wake kufuatia ushindi wake mfululizo dhidi ya bondia Alphonce Mchumiatumbo wa Tanzania na Mmarekani Shawn Miller.

Alisema rekodi za Durodoro zinaonyesha jinsi gani bondia huyo alivyo na uzoefu mkubwa katika ngumi za kulipwa kwa kushinda mapambano 34 na kupoteza manane tu wakati yeye mpaka sasa ameshinda mapambano manane, kupoteza moja na kutoka sare mara mbili.

Jongo alisema pambano hilo litamfungulia njia yake ya kucheza kwenye mikanda ya ubingwa wa Baraza la Ngumi za Kulipwa Duniani (WBC), hivyo lazima ashinde.

"Nipo tayari kwa pambano, najua uwezo wa mpinzani wangu na kamwe sitampa nafasi, natarajia upinzani mkali sana," alisema Jongo.

Durodoro aliyewasili jana alisema kuwa amekuja kuendeleza rekodi yake ya ushindi kwa kumtwanga Jongo.

Mbali ya kuwasili kwa Mnigeria huyo na mabondia wawili wa Bulgaria, Pencho Tsvetkov na mwanadada Joana Nwamerue waliwasili mapema zaidi tayari kwa mapambano hayo.

Tsvetkov atazichapa na Mtanzania Daniel Matefu katika pambano la uzito wa juu wakati Joana atazichapa na Mtanzania Leila Yazidu katika pambano la uzito wa super-light.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jackson Group Sports, Kelvin Twissa, alisema kuwa mabondia wengine Sibusiso Zingange, Antonio Maiala na Chris Thompson, watawasili leo wakati bondia kutoka Congo Brazzavile, Ardi Ndembo, atawasili kesho na kwamba tiketi zinauzwa kwa Sh. 50,000 kwa viti vya kawaida na Sh. 200,000 kwa viti maalum kwa njia ya ontapp na Nilipe. Pambano hilo limedhaminiwa na KCB Bank, Tanzania Tourist Board, DStv, Onomo Hotel, M-Bet na Plus Networks Ltd.

Michezo
Jumanne Mei 25, 2021
Nipashe




Guardiola: Aguero atajiunga na Barca UKURASA 20

KWAHERI JEMBE...



Mshambuliaji wa Manchester City, Sergio Aguero, akiagwa na wachezaji wenzake baada ya kuichezea timu hiyo mechi yake ya mwisho na kuifungia mabao mawili wakati ikiibuka na ushindi wa 5-0 dhidi ya Everton kwenye mechi ya funga msimu wa Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad juzi, ambayo timu hiyo ilikabidhiwa kombe la ubingwa. Aguero anatarajia kujiunga na Barcelona majira haya ya joto. **PICHA: MTANDAO**

# Kiwango Simba CAF chatinga bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

LICHA ya kutolewa katika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limeipongeza klabu ya Simba kwa hatua iliyofikia na kiwango cha hali ya juu ilichoonyesha kwenye michuano hiyo.

Simba ambayo ilitinga hatua ya robo fainali baada ya kuongoza Kundi A, lililokuwa na bingwa mtetezi, Al Ahly ya Misri, timu kongwe ya DR Congo, AS Vita na wakongwe Al-Merrikh ya Sudan, Jumamosi iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Kaizer Chiefs katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, lakini ikatolewa kwa jumla ya mabao 4-3, kutokana na mchezo wa kwanza ugenini kufungwa 4-0.

Akizungumza bungeni jana, Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema katika Uwanja wa Mkapa Jumamosi yalifanyika mambo makubwa.

"Kama Bunge lazima tupongeze kwa timu yetu ya Simba Sports Club kututoa kimasomaso kuweza kufika robo fainali ya Kombe la Mabingwa wa mpira wa miguu Afrika nzima, si padogo si haba.

"Kwa hiyo na wale rafiki zetu wengine nao wajitahidi badala ya ligi ya hapahapa tu, wajitahidi kidogo waige wasiogope, tunawategemea mwakani, hata Namungo wamejitahidi ni mara ya kwanza wameingia kwenye mashindano makubwa wamejitahidi. Sasa wengine mpo wapi? Badala yake tunakuwa tunashangilia wageni tu jamani," alisema.

# Yanga, Azam mlango wazi CAF

## ●●● Juhudi za Simba zafungua mlango kwa Tanzania kupeleka timu nne michuano hiyo, huku...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Yanga ikishuka Uwanja wa Kambarage mkoani Shinyanga leo kuvaana na Mwadui FC kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Azam Federation (ASFC), maarufu FA Cup, milango kwa timu hiyo kushiriki michuano kimataifa kwa ngazi ya klabu inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), sasa ipo wazi kwao pamoja na Azam FC, imefahamika.

**Bingwa wa michuano ya FA, huiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika, wakati timu inayotwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara, hubeba dhamana ya kuipeperusha bendera ya Tanzania kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.**

Kwa upande wa Tanzania, msimu huu ilikuwa na nafasi mbili kwenye michuano hiyo ya CAF, moja Ligi ya Mabingwa ambapo Jumamosi Simba ilitolewa na Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini katika hatua ya robo fainali kwa jumla ya mabao 4-3, baada ya kupoteza ugenini 4-0 na nyumbani kushinda 3-0.

Jukumu lingine kimataifa lilibebwa na Namungo FC, iliyokuwa ikiiwakilisha Tanzania kwenye Kombe la Shirikisho, lakini ikaishia hatua ya makundi baada ya kupoteza mechi zote sita katika kundi lake.

Hata hivyo, juhudi za Simba katika michuano hiyo, zimeiongezea Tanzania pointi na kufikisha 27.5 katika nafasi ya 12, ambayo inatoa nafasi ya nchi kuingiza timu nne kwa msimu mmoja wa michuano hiyo ya CAF. Kwa mujibu wa Kanuni za CAF, nchi 12 ambazo klabu zake hufanya vizuri katika michuano hiyo miwili kila msimu, hujiongezea pointi na hupata nafasi ya kuingiza timu nne, hivyo kufanya vizuri kwa Simba na Namungo iliishia hatua ya makundi kumeifanya Tanzania kupata nafasi hiyo.

Mshindani mkubwa katika nafasi hiyo ilikuwa ni Senegal, ambayo imeishia kuvuna pointi 15 baada ya timu ya ASC Jaraaf ya nchini humo juzi kutolewa na Cotton Sports ya Cameroon katika hatua ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika hivyo kuifanya Tanzania kushika nafasi ya 12.

Katika mchezo wa kwanza nyumbani, Cotton Sports iliibuka na ushindi wa bao 1-0, kabla ya juzi nchini Senegal kukubali kipigo cha mabao 2-1, hivyo kufanya matokeo ya jumla kuwa 2-2 na kuifanya kutinga nusu fainali kwa faida ya bao la ugenini huku ASC Jaraaf ikiaga rasmi na nchi yao kuishia kuvuna pointi 15.

Hivyo, kwa jinsi msimamo wa Ligi Kuu Bara ulivyo, Simba ina nafasi kubwa ya kutwaa ubingwa huo na kuiwakilisha tena nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, kutokana na kujikusanyia pointi 61 sawa na Yanga iliyopo nafasi ya pili lakini yenyewe ikiwa mbele kwa michezo minne baada ya kushuka dimbani mara 29.

Azam FC, inashika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 60 zilizotokana na michezo 30 huku ikifukuziwa kwa mbali na Biashara United yenye pointi 45 kwa mechi zake 30, hivyo timu zitakazomaliza nafasi tatu za juu zitakuwa na nafasi ya kushiriki michuano ya CAF.

Kwa mujibu wa Kanuni za Shirikisho la Soka nchini (TFF), bingwa wa Kombe la FA, ataendelea kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, huku bingwa wa Ligi Kuu na timu inayoshika nafasi ya pili, zikiwa na jukumu hilo kwenye Ligi ya Mabingwa na itakayoshika nafasi ya tatu nayo itaangukia Kombe la Shirikisho.

Simba, Yanga na Azam, licha ya kushika nafasi tatu za juu kwenye msimamo wa Ligi Kuu, pia zimetinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA, ambapo leo Yanga itakuwa ugenini dhidi ya Mwadui FC kutafuta nafasi ya kuifuata nusu fainali Biashara United ambayo juzi iliitoa Namungo FC kwa kuichapa mabao 2-0.

Azam itavaana na Rhino Rangers kesho katika robo fainali nyingine itakayopigwa Uwanja wa Kambarage, Shinyanga na mshindi wa mechi hiyo atakutana na timu itakayoshinda kesho saa 1:00 usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kati ya Simba na Dodoma Jiji FC.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >